

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

### **BUNGE LA TANZANIA**

---

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

---

### **MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 28 Oktoba, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

### **D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### **KIAPPO CHA UAMINIFU**

Mjumbe afuataye aliapa kiapo cha Uaminifu na kukaa katika sehemu yake ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera

### **TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Kumi na Mbili (uliopita), Bunge hili lilipitisha Miswada Mitatu ifuatayo:- *The Appropriation Bill, 2008, Finance Bill, 2008* na *The National Assembly Administration Bill, 2008*. Miswada hiyo niliifikisha kwa Mheshimiwa Rais ili ipate kibali chake, baada ya kupita katika hatua zote za uchapishwaji. Nafurahi kuliarifu Bunge kwamba tayari Mheshimiwa Rais ametoa kibali chake na sasa Miswada hiyo ni Sheria za Nchi kama ifuatavyo:- *The Appropriation Act, 2008* sasa inakuwa ni Sheria ya 12 ya Mwaka 2008, *The Finance Act, 2008* ni Sheria Namba 13 ya 2008 na *The National Assembly Administration Act, 2008* ni Sheria sasa Namba 14 ya Mwaka 2008. Ahsanteni sana! (*Makofi*)

### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 1

**Mishahara ya Watendaji wa Vijiji na Kata**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA (K.n.y. MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO)** aliuliza:-

Kwa kuwa mishahara ya Watendaji wa Vijiji na wa Kata walioanza kazi zamani inafanana na ile ya walioanza kazi baada yao hata pale ambapo ni darasa la Kumi na Mbili:-

- (a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha kero hiyo inaondolewa?
- (b) Je, ni nini *career path* ya Mtendaji wa Kijiji na Kata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utendaji katika ngazi mbali mbali ikiwa ni pamoja na Vijiji na Kata, Serikali ilitoa Waraka wa Maendeleo ya watumishi Namba 29 wa mwaka 2003. Waraka huu uliainisha sifa za msingi zinazotakiwa kwa ajira za Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata. Kiwango cha chini cha Elimu kilichoainishwa na Waraka huu ni Elimu ya Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ilifanya uamuzi wa busara kwa kuendeleza ajira za Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata ambao hawakuwa na Elimu ya Kidato cha Nne.

Wahusika walitakiwa kujiendeleza ili kuweza kukidhi masharti ya ajira zao kwa mujibu wa Waraka uliotolewa. Sambamba na kuendeleza ajira zao, wasingeweza kupanda katika ngazi nyingine ya mishahara hadi pale watakapokuwa wamejiendeleza na kupata Elimu iliyoelekezwa (Kidato cha Nne).

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Watendaji walioanza kazi zamani wanaweza kufanana mishahara na wale walioanza kazi baada yao kwa sababu wale wa zamani walipanda mishahara kwa muda wao kazini na wanaoanza sasa wanakidhi vigezo vilivyowekwa.

(b) Watendaji wa Vijiji na Kata kama ilivyo kwa Watumishi wengine wa Umma, Miundo yao ya maendeleo katika utumishi iko katika ngazi mbali mbali. Kwa mfano, Mtendaji wa Kijiji huanzia ngazi ya Mtendaji Kijiji Daraja la III mpaka Afisa Mtendaji wa Kijiji Mkuu na kulipwa mishahara wa ngazi ya *TGS F*. Mtendaji wa Kata huanzia ngazi ya Mtendaji Kata Daraja la III mpaka Afisa Mtendaji wa Kata Mkuu na hulipwa mishahara ngazi ya *TGS G*.

Mheshimiwa Spika, Watendaji hawa wanaweza kujiendeleza au kuendelezwa na wakawa na sifa za kitaalam ngazi za Cheti, Diploma, Shahada, Stashahada na Shahada za Uzamili hata Shahada za Uzamivu (*PhD*) katika fani mbali mbali. Hivyo watendaji wanaweza kubadilishwa vyeo kulingana na kiwango na aina ya elimu waliyonayo baada ya kujiendeleza. Mheshimiwa Spika, *Career Path* ya Maafisa hawa ipo wazi. Hivyo, ni jukumu lao wenyewe kujituma na waajiri wao kuona umuhimu wa kuwaendeleza ili wapandishwe vyeo chini ya Muundo wao wa Utumishi na hata kujaza nafasi zingine za Uongozi na Uteuzi katika Utumishi wa Umma.

**MHE. DR. CHRISSANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwea kuwa Vijiji tulivyonavyo Tanzania ndio kitovu cha maendeleo ikiwemo kilimo na mambo mengine. Na Vijiji vingi vina idadi ya watu mpaka 4000/5000/6000. Je, Serikali itakubaliana kwamba ingekuwa ni wakati muafaka sasa kutazama upya kabisa kiwango na uwezo wa ajira ya Watendaji wa Kata na Vijiji ili vifanane na kuweza kuongoza Vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mzindakaya kwamba kwa majukumu ambayo tumejiwekea sasa hivi kwa maana ya kuendeleza Vijiji vyetu na kuelekeza mtizamo wetu katika Vijiji, tuna haja ya kuwa na watu ambao wana kiwango cha juu cha elimu cha kuweza kuelewa kwamba ni mambo gani yanayotakiwa kufanyika kule na ndio maana kwa utaratibu tuliojiwekea katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, sasa hivi tunacho Chuo chetu cha Hombolo ambacho kinafanya kazi hiyo ya kuhakikiha kwamba tunakuwa na watumishi walioko katika ngazi ya Vijiji na Kata wanaokidhi haja hiyo ambayo anazungumzia Mheshimiwa Chrisant Majiyatanga Mzindakaya.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda uliotolewa kupitia Waraka wa Mwaka 2003 sasa umekwisha; na kwa kuwa Watendaji hawa ndio injini kubwa ya maendeleo katika nchi yetu. Je, Serikali iko tayari sasa kufanya tathmini kuona ni wangapi wamejiendeleza na kuhitimu kidato cha nne na kama hawajafika, Serikali inachukua hatua gani kwa wale walioshindwa kuhitimu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, anachozungumza ni sahihi kabisa. Muda ulitolewa na kwa kweli wale ambao wameshindwa kufikia hatua hiyo, sasa hivi tuko katika mchakato huo wa kuhakikisha kwamba tunafanya tathmini. Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama tulivyoeleza katika jibu la Msingi hapo awali, nia na shabaha ni kusema wale ambao walikuwa wamejenga uzoefu pamoja na kwamba walikuwa hawakufika kidato cha nne, hebu tutumie uzoefu wao. Lakini wakati huo huo tuwatake wao wajiendeleze wao wenyewe wakafikia katika ngazi hiyo ya kidato cha nne kwa maana ya darasa la kumi na mbili. Sasa hivi tunafanya hiyo tathmini na tunaendelea.

Nadhani anachotusaidia hapa, ni kwamba anatusaidia kwamba kama tutakuwa bado na mtu ambaye yuko, na hawezi kabisa kubadilika sana kiasi ambacho mtu hawezi kubaki pale na hesabu za kikwetu, halafu ukasema huyu unaendelea naye.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaona kwamba kuna haja ya kufanya hiyo tathmini. Kuhusu kwamba ni hatua gani itakayochukuliwa, sasa hatua itakayochukuliwa ni kwamba tutamtema tu mtu huyo.

Lakini sasa hili ni jambo ambalo tunatakiwa Serikali kulitafakari wote kwa pamoja na kukubaliana kwamba tunaona kwamba kuna umuhimu wa kuwaondoa wale ambao wanaonekana kwamba hawajakidhi hiyo haja.

Na. 2

### **Mji wa Ngaramtoni ya Juu kuwa Mji Mdogo**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER (MHE. ELISA D. MOLLEL)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Ngaramtoni ya Juu unakua kwa kasi sana na kwamba Serikali imeishapima viwanja vya makazi kwa nia ya kuwa na ujenzi unaoendana na mipango Miji na huduma za jamii.

Je, ni lini Mji huo utakubaliwa kuwa Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Ngaramtoni ya Juu linakua kwa kasi. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali iliona hilo na ndio sababu katika Tangazo lake Na. 168 la tarehe 29 Aprili, 1994 kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na

Maendeleo ya Makazi ilitangaza eneo la Ngaramtoni ya Juu kuwa eneo la Mipango Miji (*Planning Area*). Takriban asilimia 30 ya Mji wa Ngaramtoni una michoro ya Mipango miji.

Hata hivyo asilimia 70 iliyobakia ya Mji huo bado ni eneo la Mamlaka za Vijiji sita (6) na haina michoro ya Mipangomiji. Ili Halmashauri iweze kuingia na kupanga Mji Mamlaka ya Vijiji vilivyopo katika eneo hilo itatakiwa ifutwe. Kwa sasa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha imeishaanza mchakato wa kufuta jumla ya Mamlaka za Vijiji sita ili kutimiza taratibu za kufanya eneo hilo kuwa la Mipango Miji. Mchakato huo utakapokuwa umekamilika, eneo la Ngaramtoni ya Juu litakuwa na michoro ya Mipango Miji na ndipo uwezekano wa kutangazwa kuwa Mji Mdogo utakapofikiriwa.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kukamilisha mchakato wa kuifanya Ngaramtoni ya Juu kuwa Mji Mdogo kwa kuhakikisha kwamba mchakato huo unapitia katika vikao halali vya Halmashauri kabla ya kuwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ili eneo hilo litangazwe kuwa Mji Mdogo.

Hivyo basi, lini eneo hilo litakuwa Mji Mdogo, inategemea sana kasi itakayotumika kukamilisha mchakato. Napenda kuchukua nafasi hii kuishauri Halmashauri ya Arusha pamoja na wananchi wake kuharakisha mchakato huu ili eneo la Ngaramtoni ya Juu litangazwe kama Mji Mdogo na kama Mheshimiwa Mbunge anavyoomba.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili kwa niaba ya Mheshimiwa Elisa Mollel. Kwa kuwa Mji wa Ngaramtoni ni Mji unaokua sana kama alivyosema Naibu Waziri na ni Mji unaokua sana na ni Mji ambao uko karibu sana na Mji wa Arusha na imekwishaungana sasa na Mji wa Arusha. Nadhani kuwa Mji mdogo ni muda uliopita, kwa sasa inastahili kuwa Mji.

Je, Serikali haioni kwamba ni afadhali waanze sasa mipango hiyo, ijulikane wananchi wanaolipwa fidia wale wanaondoshewa? Swali la pili, kwa kuwa Mji wa Ngaramtoni ni Makao Makuu ya Wilaya ya Arusha Vijijini, kwa sasa haistahili Mji huo kutangazwa kwa wakati huu kuwa Mji kuliko kusubiliwa tena kuwa Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mimi nadhani Mheshimiwa Lekule Laizer, mimi namuelewa anachosisitiza hapa ni kupatikana kwa Mji Mdogo wa Ngaramtoni, *that is the bottom line*, ndicho anachotaka pale. Na anachosema kwamba Je, kwa hali hiyo ambayo ameieleza, hatuoni kwamba kuna haja sasa ya kutangaza moja kwa moja?

Mheshimiwa Spika, mchakato mzima wa kusema hapa pawe Mji Mdogo unatokana na Halmashauri yenyewe ya Ngaramtoni kwa maana ya Halmashauri ya

Arusha. Mtakumbuka kwamba Serikali iliwahi kusema hapa kwamba mahali popote pale ambapo pameanzishwa Makao Makuu ya Wilaya, kwa kweli ni kama vile tayari mchakato huo umeishaanza kwa maana panakuwa sasa ni Mji Mdogo.

Lakini, huo Mji mdogo haupatikani hivi hivi tu bila wenyewe wenye Mji Mdogo huo kutoa ridhaa na ridhaa hiyo inapatikana kupitia Baraza la Madiwani na kupitia kwenye vile Vijiji tunavyozungumza na hatimaye inakuja kwa Waziri mwenye dhamana ambaye ndiye sasa kwa kufuata ule mchakato ambao nimezungumzia, anatamka kwamba hili eneo sasa anakubali liwe ni eneo la Mji mdogo.

Mheshimiwa Spika, anasema Makao Makuu yako pale Ngaramtoni, ni kweli kabisa. Lakini, kama nilivyosema, haiwi ni *automatic*. Yaani siyo kwamba ukishakuwa hivyo ulivyo hivyo, basi inakuwa. Kwa hiyo, mimi nataka kurudisha tena jambo hili kule kule Ngaramtoni kwa Mheshimiwa Lekule Laizer. Pamoja na Mheshimiwa Mollel, wake sasa watupitishie haraka haraka na sisi kama tulivyoahidi hapa, tukipokea tutalifanyia kazi mara moja. Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa utaratibu huu wa kupanga miji katika Halmashauri zetu ni maeneo mengi katika nchi hii; na ukizingatia mapaka hivi sasa utakuta kwamba katika Makao Makuu ya Miji katika Wilaya zetu, bado maeneo yale Viongozi wake wanajulikana kama Wenyeviti wa Serikali za Vijiji. Lakini wako katika Mji au Makao Makuu ya Wilaya. Je, hali hii Serikali inaeleza na hatimaye kutambua kwamba sasa ile ni Miji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na yeye kabisa kwamba maeneo mengi katika Tanzania, hata hapo kwako, hata kwangu kule Sanya Juu yanafanana hivyo. Lakini, huwezi ukatoka pale, ukasema kwamba kwa vile hapa pameishafanana fanana na Mji Mdogo kwa hiyo napabatiza leo kwamba kutoka sasa Mwenyekiti wake atakuwa anitwa Mwenyekiti wa Mtaa kwa sababu tu pamekuwa na mazingira hayo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, bado ni utaratibu, hata pale kwako Urambo, mtatakiwa wale watu wa Urambo pale mkae, mkubaliane, msemi kwamba sisi hapa tumeridhika kwamba pawe ni Mji Mdogo.

Labda nifafanue kidogo hapa kwa sababu linajirudiarudia. Ni kwamba pale pana *politics* na *economics* zake zinajitokeza pale, ukianza wewe kupima pale bila kupata ridhaa ya wale wenyewe walioko pale, baadaye ukasema hapa ni Mji Mdogo kwa hiyo kutoka sasa huyu atakuwa haitwi Mwenyekiti wa Kijiji, ataitwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaaa, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa pale anatamka wakati unapokuwa na Mamlaka ya Mji Mdogo wa eneo hilo, ndipo unapomwista hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa taarifa hiyo! Swali la mwisho la nyongeza, Mheshimiwa Zitto!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kuna matatizo maeneo mengi ambayo tayari Miji midogo imeanza na mfano dhahiri ambao tumeupata hivi karibuni ni katika Mji Mdogo wa Mugumu, Serengeti ambapo tayari Mji Mdogo umeundwa na Madiwani wanatakiwa Madiwani watatu kutoka kwenye Halmashauri ya Wilaya kuingia kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo.

Katika Kata ya Mugumu Mjini, Diwani anatoka Chama cha *CUF*, lakini Halmashauri ya Wilaya imeteua Madiwani watatu, yule Diwani wa pale Mjini mwenye Mji Mdogo hayumo kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo. Serikali inatoa kauli gani kuhusu hilo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli suala hili limenifikia Ofisini kwangu, limefikishwa na Mheshimiwa Jecha pamoja na Mheshimiwa Slaa, tunalifanyia kazi na tutawajibu.

Na. 3

**Kuongeza Mapato kutokana na *Deep Sea Fishing Authority***

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la *Deep Sea Fishing Authority* ni la Muungano na ni mojawapo ya migodi mikuu ya uchumi wetu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu na mfupi wa kuvuna uchumi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Col. Saad Mgeni, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwenye Bahari Kuu eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 223,000 ili kuongeza mapato ya wananchi na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma hii, Wizara yangu inaendeleza mchakato wa kuanzisha chombo cha Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari Kuu (*The Deep Sea Fishing Authority*) kwa mujibu wa sheria. Sheria ya *The Deep Sea Fishing Authority Act, Cap. 388* ya mwaka 1998 imefanyiwa marekebisho.

Marekebisho hayo yalipitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 5 Februari, 2007 na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 30 Machi, 2007 na ilianza kutumika rasmi tarehe 1 Juni, 2008.

Kwa kuwa suala la uvuvi kwenye bahari si la Muungano, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inaandaa Kanuni za kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuandaa Kanuni Kanuni za Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari Kuu tayari umeanza kwa kuteua Kamati Maalum ya Maafisa wa Serikali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wenye taaluma na uzoefu wa masuala ya uvuvi na sheria kufanya kazi ya kutengeneza Kanuni.

Tayari Hadidu za Rejea zimeandaliwa na kazi inaendelea. Aidha, Ofisi za awali kwa ajili ya ya Makao Makuu ya Mamlaka hiyo tayari zimepatikana katika Manispaa ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mfupi wa kuvuna rasilimali za uvuvi umejumuisha uboreshaji wa masharti ya leseni za uvuvi. Kwa kutumia sheria ya uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 kwa Tanzania Bara, masharti hayo yanajumuisha meli kuegesha na kushusha mazao ya uvuvi katika bandari za Tanzania, kutokumwaga baharini samaki wa aina nyingine ambao siyo walengwa, kuajiri wavuvi Watanzania, Nahodha kuwaweka maafisa waangalizi wa Serikali kwenye meli, kila meli kutakiwa kuwa na vifaa vya *vessel monitoring system* na kutoa taarifa za takwimu za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu Serikali imeipa Mamlaka ya Kusimamia uvuvi katika bahari kuu majukumu ya kuweka taratibu za usajili wa vyombo,



viwango vya leseni za uvuvi, kudhibiti nguvu ya uvunaji na kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi kwenye bahari kuu.

Katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka itahakikisha kuwa uvuvi unakuwa endelevu na kulipatia Taifa manufaa yanayostahili kutoka kwenye rasilimali za uvuvi katika bahari kuu.

**MHE. COL.. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake zuri la kutia matumaini. Lakini, nina swali dogo kabisa la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri anaelewa kwamba hivi sasa samaki wanaibiwa sana huko Bahari Kuu? Na kama anaelewa.

Je, kuna mpango gani wa udhibiti wa samaki hao ili kudhibiti pato letu la Taifa? Ahsante sana!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir , Mbunge wa Fuoni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo?

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumegundua kwamba rasilimali zetu zinaibiwa na kuna meli nyingi za kigeni ambazo zinakuja na kuvua huko, sasa tunachukua hatua ili kuhakikisha kwamba bahari yetu siyo shamba la Bibi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa meli sasa hivi zinatakiwa kuja kwenye bandari ya Tanzania kwa ajili ya kupata huduma kabla hazijaenda huko kwanza tuzitambue halafu zichukue mafuta kutoka nchini kwetu, maji na chakula, na vile vile lazima waje tuwape watu ambao wataambatana nao kwenda kuvua huko na hao ndiyo watakaotuletea ripoti. Baada ya hapo wanatakiwa waje kwenye bandari zetu watie nanga na tuangalie kuna nini mle ambacho wamevua na waweze kupata huduma muhimu kama chakula, maji na mafuta na kama kuna Samaki wengine ambao zamani walikuwa wanawatupa huko baharini baada ya kuvua sasa hivi tunataka watuletee hapa ili waweze kutumiwa na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata ada za leseni nazo tumejaribu kuzibadilisha, zamani mtu alikuwa anakuja analipa dola 16,000 kwa mwaka lakini tunajua kwamba uvunaji wetu ni wa miezi mitatu. Sasa hivi tumesema mtu akitaka tumegeuza leseni, kwanza meli za nje zinatakiwa kulipa USD 12,000 kwa miezi mitatu. Kama anataka kwa mwezi mmoja mmoja atalipa dola elfu tano na raia wa Tanzania atatakiwa kulipa dola 4,500 kwa miezi mitatu na kama atataka kwa mwezi atavua kwa dola 1,500.

Mheshimiwa Spika, lakini meli aina ya *long liner* sasa zinatakiwa kulipa dola za Marekani 32 na kama atataka kulipa kwa kila mwezi atalipa dola 3,500 hii yote ni kuhakikisha kwamba Samaki wetu hawaibiwi huko baharini. Sasa hivi meli yeyote itakayopatikana bila kutimiza masharti inachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nilivyosema kwa muda mrefu sasa tunaandaa kanuni na baada ya hizo kanuni kukamilika *Deep Sea Authority* itahakikisha mambo yanaenda vizuri.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo inaonekana ana ushirikiano wa karibu baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar, tatizo nililozungumza kwenye swali la Msingi ni uvuvi wa Bahari Kuu. Lakini napenda nimhakikishie kuwa kuna meli za kigeni zinazovua katika mwambao wa Pemba Kaskazini karibu kabisa na visiwa.

Je, hivi Serikali masuala haya haiyaoni na sheria zinapita hivi inachukua muda gani kuwakabili wezi hawa ambao wanaidhulumu rasilimali ya msingi ya Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunakubaliana kwamba kuna haya matatizo na matatizo tunakosa vyombo, ukichukulia nchi kama Namibia wao wanatumia *Navy, South Africa* wanatumia *Garnishing*, sisi kwa sasa hivi hivyo vyombo hatuna na tunajaribu kusema kwamba ukiwa huko kwanza ni lazima uje Tanzania tukufahamu na kama hupo tumeanzisha doria kwa sasa ambazo tukipata meli yeyote ile inachukuliwa hatua kama haijaja kutia nanga na kutujulisha kwamba inavua.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kilichosababisha haya yote ni kwa sababu tu kwamba vyombo vya kudhibiti uvuvi huo haramu ilikuwa hakuna lakini maandalizi yanafanyika ambapo baada ya muda mfupi hili tatizo litatatuliwa vizuri.

Na. 4

### **Sheria ya kulinda Unyanyasaji Mifugo**

**MHE. AMEIR ALI AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi ya wafugaji na kuna wafugaji wengi wa mifugo mbalimbali kama Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Kuku na kadhalika, na kwa kuwa, kumejitokeza vitendo vya kuwauza sokoni, hali ambayo husababisha maumivu, uchovu na vifo kwa wanyama hao:-

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusu vitendo hivi vya unyanyasaji wa mifugo?

(b) Je, nchi yetu ina sheria yeyote iliyowekwa kulinda usalama wa mifugo?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo;

Serikali inatambua na inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa vitendo vya kuning'iniza kuku kwenye baiskeli ni miongoni mwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa mifugo.

Vitendo vya mateso na maumivu kwa wanyama vinabainishwa na sheria kuwa makosa ya kisayansi vinaathiri uzalishaji na ubora wa bidhaa hususani wa nyama.

Nyama itokanayo na wanyama walioteswa hushuka ubora na huharibika haraka kutokana na kupungua kwa viwango vya *glycogen* na *Lactic Acid* kwenye misuli.

Kwa kutambua uhusiano wa ustawi wa wanyama uzalishaji na ubora wa mifugo Ibara ya 3.19 ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 inahimiza juu ya Ustawi wa wanyama,(Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahamasisha na itaimarisha utoaji wa huduma na kuratibu utekelezaji wa misingi ya ustawi wa wanyama ) katika kutekeleza azma hii.

Serikali inashirikiana na Asasi za Kiraia zinazojihusisha na ustawi wa wanyama zikiwemo *Tanzania Society for Prevention of Cruelty to Animals (TSPCA)*, *Tanzania Animal Protection Organisation(TAPO)*, *Tanzania society for animal Welfare (TAWESO)* *Arusha Society for Protection of Animals(ASPA)*, *Sea Sense, Root and Shoots*, *Dar es Salaam Animal Haven(DAH)* na *World Society for Protection of Animals (WSPA)* kwa *Tanzania BARA*.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Tanzania ina mifugo mingi, aidha nchi yetu ina sheria ya kulinda wanyama na 153 ya mwaka 1962

(*Animal Protection ordinance Cap. 153*) Sehemu ya tatu (3) ya sheria hii inabainisha vitendo vya kuning'iniza, kupiga, kujeruhi na kuwatesa wanyama kuwa ni ukatili na ni makosa. Kutokana na sheria hii kupitwa na wakati na upana wa dhana ya ustawi wa wanyama inayozingatia maeneo ya msingi kupewa wanyama (*Universal Fundamental Freedoms*), Serikali imeandaa na kuwasilishwa Bungeni Muswada wa Sheria ya Ustawi wa wanyama (*The Animal Welfare Act*) pamoja na mambo na kupunguza vitendo ambavyo Mheshimiwa Mbunge wamevitaja ikiwa ni pamoja na kuwaningi'iniza kuku kwenye baiskeli.

**SPIKA:** Hivi ukatili ni kuning'iniza kwenye baiskeli tu?

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza;

(a) Kwa kuwa, sheria ipo na haikufuatwa na asasi zipo lakini zipo kimya na kitendo hiki bado kinaendelea, Serikali inatoa kauli gani katika kipindi hili cha mpito kuelekea katika sheria mpya tuliyojiwekea hapa Bungeni?

(b) Sheria hii ambayo inaondoshwa ilikuwa inatoa hukumu gani kwa anayebainika kunyanyasa au kudhalilisha mifugo hii?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mpito tumesema kuna sera ya mifugo ambayo kama sasa hivi utapatikana sheria inachukua mkondo wake, lakini bado tunafuata ile sheria ya mwaka 1926 ambayo faini yake ni ndogo sana tunachokuwa tunafanya ni kuwaonya kwa sababu faini ni kidogo sana na imepitwa na wakati. Sasa hivi tunapokwenda kwenye sheria ya sasa itakuwa ni msumeno. Kwa sasa hivi tunamakosa ambayo tumebainisha ambayo ni makosa kumi, yapo makosa manane, kwanza tutakuwa na Inspekta katika sheria mpya ambapo akikupata anakupa faini ya papo kwa papo shilingi elfu ishirini kama itapitishwa na Bunge. Lakini kama utaonekana unakaidi unaning'iniza wanyama, unapelekwa mahakamani na faini ya sasa itakuwa ni kufungwa miezi sita ama kupigwa faini shilingi milioni moja ama pamoja, kwa hiyo Serikali imepania kabisa ku-*protect* wanyama wetu siku zinazokuja.

Na. 5

### **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara kuwa cha Kimataifa**

**MHE. RAYMOND A. MROPE (K.n.y. MHE. JUMA A. NJWAYO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kiwanja cha ndege cha Mtwara kinatumika pia kwa ndege kutoka Komoro na Msumbiji:-

(a) Je, ni sifa zipi zinzofanya kiwanja cha ndege kuwa cha Kimataifa?

(b) Je, Serikali ina Mpango gani wa kufanya kiwanja cha Ndege cha Mtwara kiwe cha Kimataifa?

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE (K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOBINU) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kiwanja cha ndege kiwe cha kimataifa kinatakiwa kiwe na sifa zilizowekwa na shirika la Kimataifa la Kusimamia Usafiri wa Anga Duniani (*International Civil Aviation Organisation-ICAO*). Sifa hizo ni:-

(i) Kiwe kimeteuliwa na nchi husika kuwa kituo cha kuingia na kutoka *exit and (entry point)*.

(ii) Kiwe na Miundombinu madhubuti hususani njia ya kurukia na kutua ndege (*runway*) kiwe na vifaa kama vile taa za kuongozea ndege ili ziweze kutua au kuruka kwa usalama wakati wowote, yaani usiku na mchana.

(iii) Kiwe na huduma za uhamiaji, forodha, afya na polisi zinazotolewa kwa saa 24 kwa siku ili abiria, mizigo au vifurushi vinavyoletwa na ndege viweze kuingia au kutoka nje ya nchi wakati wote.

(iv) Kiingizwe kwenye orodha ya viwanja vinavyokaguliwa na shirika la Kimataifa la usafiri wa anga Duniani (*ICAO*) na kiwe tayari kukaguliwa na shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, kiwanja cha ndege cha Mtwara ni moja kati ya viwanja ambavyo vimeteuliwa kama cha kuingia na kutoka (*Exit and Entry Point*) na kinahudumia ndege zinazoingia na kutoka nchini. Aidha miundombinu ya kiwanja inaruhusu ndege kutua na kuruka kwa usalama. Hata hivyo bado kiwanja cha ndege cha Mtwara si cha Kimataifa kwani huduma za Uhamiaji forodha, afya na Polisi hazitolewi kwa saa 24 kwa siku na miundombinu yake hairuhusu ndege kutua muda wote hasa usiku.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kiwanja cha Ndege cha Mtwara katika Maendeleo ya Kanda ya Kusini chini ya Mtwara *Corridor* na kipo katika Programu ya Kitaifa ya Uwekezaji kwenye miundombinu (*Transport Sector Investment Programme*) ambayo inajumuisha pia viwanja vingine vya biashara ya ndege hapa nchini.

Kwa sasa Serikali kupitia mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekamilisha mpango kamambe wa kiwanja cha ndege cha Mtwara (*Mtwara Airport Master Plan*) na inaendelea kutafuta rasilimali za kuendeleza miundombinu na majengo ya kiwanja ili yawe ya kisasa. Ni matumaini ya Serikali kuwa, kadri miundombinu ya kiwanja cha Ndege cha Mtwara itakavyoendelea kuboreshwa hatima yake kiwanja hicho kitaweza kufikia hadhi ya kuwa kiwanja cha ndege cha Kimataifa.

**MHE. RAYMOND A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Naibu Waziri kwa kutoa majibu fasaha katika suala hili la Mheshimiwa Njwayo, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa, Mtwara hivi sasa kuna uhakika wa umeme kuliko eneo lolote Afrika na kutokana na hali hii kwa nini taa za kuongozea barabara katika kiwanja cha Mtwara haziwekwi na lini sasa Waziri anaweza akaweka, kwa sababu ni suala ambalo ni la uhakika sana umeme upo mwingi sana.

(b) Kuna upanuzi unaofanyika hivi sasa katika kiwanja chetu cha Mtwara lakini Waziri atakubaliana nami kwamba unakwenda kwa mwendo wa Jongoo.

Je Waziri anaweza kutuhakikishia ni lini kazi ya upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mtwara utakamilika ili uweze kuwa wa Kimataifa kwa upesi iwezekanavyo?

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE (K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi ina chanzo cha umeme ambacho ni cha uhakika na kwa hiyo katika suala la kuhakikisha kwamba kuna umeme katika kiwanja cha Mtwara ni moja kati ya mambo ambayo nimeyaeleza hapa katika jibu la msingi ya kwamba Miundombinu pale inaendelea kuboreshwa na kama alivyoeleza katika swali la pili kwamba upanuzi bado unaendelea kwa hiyo hapa tunachozungumzia ni suala tu la kwamba tunakusanya uwezo wetu ili kuhakikisha kwamba miundombinu ya pale inaendelezwa ikiwa ni pamoja na hii ya taa lakini siyo hiyo ya taa tu lakini ni pamoja na kuwekewa uzio katika kiwanja cha Mtwara ili kiweze kuboreka zaidi

Mheshimiwa Spika, upanuzi unaoendelea hivi sasa kama unakwenda kidogo kidogo pengine inawezekana ni katika upatikanaji wa nyenzo tu kama nilivyokuwa nimesema lakini nataka nimhakikishie kwamba kwa sababu azma ipo ya kuhakikisha kiwanja hiki kiweze kuendelezwa na kwa sababu kipo katika ile *master plan* tutaendelea kuisimamia kwa karibu kuhakikisha kwamba uwanja huo unaboreka na kufikia kiwango ambacho kilikuwa kikikusudiwa.

Na. 6

### **Kupaki Magari Makubwa eneo la Mbezi-Kibaha**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, magari makubwa ya mizigo yanapaki kandokango ya barabara ya Morogoro maeneo ya Mbezi hadi Kibaha husababisha ajali nyingi katika barabara hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuandaa sehemu ya kupaki magari makubwa ili kuepusha ajali zinazoweza kutokea katika maeneo hayo?

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE (K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kwanza napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa kituo cha kuchunguza magari makubwa yenye mizigo na madogo yaendayo nje ya Nchi kinachosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kilichopo Mbezi kimekuwa kikileta usumbufu mkuwa kwa watumiaji wa barabara ya Morogoro kutokana na magari hayo kuegeshwa pembezoni mwa barabara.

Kitendo cha magari hayo makubwa kuegeshwa pembezoni mwa barabara kimekuwa pia ni chanzo cha uharibifu wa kingo za barabara na wakati mwingine chanzo cha ajali katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali kwa kupitia Kikosi cha Polisi cha Usalama Barabarani (*Traffic Police*) kimeendelea kusimamia eneo hilo kwa karibu, kwa lengo la kuongeza na kuelekeza magari yanayopoegeywa ili kuepusha ajali zinazoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli za Mamlaka ya Mapato Nchini na suala zima la usalama barabarani, Wizara yangu kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Mamlaka ya Mapato Tanzania tunaendelea na Mchakato wa kutafuta eneo muafaka ndani ya Halamashauri ya Kibaha litakaloweza kutumika na *TRA* kwa shughuli za ukusanyaji wa mapato.

Lengo la kutafuta eneo moja jipya ni kuondoa kabisa kituo cha kuchunguza magari cha Mamlaka ya Mapato Tanzania kilichopo Mbezi.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa, tathmini ya tarehe 25 mwezi wa Kumi 2008 Morogoro ajali nyingi zinatoka Kibaha Chalinze na Morogoro kwenyewe na ukizingatia maeneo ya Kibaha mpaka Mbezi yale malori ikifika muda wa jioni yanaziba kabisa njia, wale wanaotoka mikoani njia inakuwa ndogo.

Kwa kuwa, hali hiyo ni kero kwa wananchi Serikali inachukua hatua gani kwa haraka ili kuweza kuwasaidia wananchi kutokana na ajali hizo?

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE (K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niseme kwamba nilipokuwa

najibu swali la msingi hapa nimekiri kwamba ule uegeshaji wa magari pale Mbezi ni kero na kusema kweli wakati mwingine unasababisha ajali. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba Serikali inakiri kwamba liko tatizo hilo na hatua za muda mfupi ni hizo ambazo tunaharakisha kwamba wenzetu wa Usalama Barabarani wanakuwepo pale kuweza kutoa maelekezo hayo.

Kikubwa zaidi ninachotaka kusema hapa pengine ni kuwaelimisha watumiaji wote wa barabara wakiwemo madereva pamoja na watumiaji wengine kuhakikisha kwamba wanakuwa waangalifu na hasa ukizingatia kwamba katika wiki ya nenda kwa usalama wiki hii kauli mbinu ulikuwa ni kwamba ajali hizi zinaweza zikaepukika ikiwa kila mmoja atachukua tahadhari. Lakini suluhisho la mwisho katika kituo hiki nilisema kwamba baadaye tunatakiwa tukihamishe kiende mahali pengine ambapo msongamano wa magari hautakuwa mkubwa kama ilivyo hivi sasa.

Na. 7

### **UUNDAJI WA SERA YA UHAMIAJI**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (K.n.y. MHE. MWINCHOUM A. MSOMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mpango wa kuandaa upya Sera ya Uhamiaji itakayobainisha masuala ya raia, vitambulisho vya uraia na ukaazi katika mazingira mapya ya kuendeleza ushirikiano katika *SADC* na Jumuiya ya Afrika Mashariki:-

(a) Je, uandaaji wa Sera hiyo umeanza kama bado nini kinakwamisha sera hiyo?

(b) Je, Mpango huo unaendeleaje ikiwa umeshaanzishwa?

(c) Je, mchakato wa kuanzisha na kutoa vitambulisho vya uraia umefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali hili nilikuwa Jimboni kwangu wananchi wa Jimbo la Bukoba Mjini wamenituma salamu zao kwako na nafikiri wanaona kwamba nimezifikisha lakini pia wamenipa salamu kwa Wabunge wote na kuwatakia kheri katika shughuli za Bunge katika Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Spika, Mchakato wa uundaji wa Sera ya uhamiaji umeshaanza na unaendelea, mara sera hiyo itakapokamilika Bunge lako Tukufu litajulishwa.

Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu swali Na. 468 la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhanya, katika Mkutano wa 12 wa Bunge lako Tukufu nilieleza kwamba zabuni ya kumpata Mkandarasi wa mradi huo ilikuwa katika uchambuzi wa awali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba uchambuzi wa zabuni hiyo umekamilika mwezi Septemba, 2008 na taarifa ya tathmini ya uchambuzi (*Evaluation Report*) huo imeshapokelewa na inafanyiwa kazi

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, pamoja na tathmini ambazo Wizara imekwishafanya na hususani katika suala zima la vitambulisho ambalo limechukua muda mrefu sana.

Je, Serikali inaweza ikaliambia Bunge hili kwamba vitambulisho hivyo hivi sasa vitaweza kutumika kwa *Multi purpose* kwa maana kwamba kutumia katika masuala ya Uchaguzi, katika masuala ya leseni ya magari na katika matumizi mengine muhimu katika nchi hii?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumhakikishia pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba vitambulisho vitakavyotolewa vitakuwa ni *multipurpose* na ni nia ya Serikali kwamba vitambulisho hivyo vitatumika kama leseni za udereva, kama vitambulisho kwa ajili ya uchaguzi na aina mbalimbali ya vitambulisho ambavyo vitahitajika hapa nchini.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona ili niulize swali nyongeza.

Je, Serikali inajua kwamba kuchelewa kuletwa kwa sera hii ya uhamiaji ndiko kulikopelekea baadhi ya magereza yetu kujazana wahamiaji haramu wakiwemo Waethiopia 111 kwenye gereza la Luanda, Mbeya na ni lini Waethiopia hao watapelekwa kwao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nisikubaliane naye kwamba ucheleweshaji wa sera hii ndiyo imekuwa sababu kubwa ya Waethiopia kuwa wengi katika mahabusu au wahamiaji haramu kuwa wengi katika mahabusu kuwa wengi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wahamiaji haramu wanatokana na matatizo katika nchi jirani na hili ni suala tofauti na wanapokuja wakiingia Tanzania wengi wanarejeshwa walikotoka na tunaziomba Serikali husika ambazo zina matatizo wawachukue watu wa Taifa lao na hii kwa kweli imekuwa inafanyika.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa Sera hii naweza nikasema kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mpesya kila tunapopiga hatua yamekuwa yanajitokeza mambo mbalimbali kwa sababu imebidi twende na sera ambayo itaendana na masuala yote mazima katika nchi za *SADC* na katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na ninafikiri katika matatizo hayo kwamba kumekuwa na ucheleweshaji lakini nataka kumhakikishia tumefikia hatua kubwa sana na tumekwenda mbele tupo katika hatua za mwisho kukamilisha suala hili na suala la mtazamo mzima katika suala la uhamiaji katika nchi hii.

Na. 8

### **Vitambulisho vya Uraia vya Kudumu**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mkakati wa kuwapatia raia wake vitambulisho vya Uraia vya kudumu kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010; na kwa kuwa; wakati huduma Tume ya Uchaguzi inaendesha zoezi la kuandikisha na kutoa vitambulisho vya kupitia kura; na kwa kuwa, ni busara fedha nyingi zikaelekezwa katika mpango wa vitambulisho vya kudumu:-

(a) Je, Serikali haioni kama kufanya hivyo na kuacha mara moja zoezi la Tume ya Uchaguzi kuandikisha wapiga kura?

(b) Je, ni nchi ngapi hutumia Pasipoti au *Identity Card* kwa ajili ya kupiga kura?

(c) Je, Serikali itatoa kiasi gani cha fedha kama ikitumia utaratibu huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu a, b, na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Vitambulisho vya Taifa umelenga katika kuweza kuwatambua Watanzania wenye umri wa kuanzia miaka Kumi na Minane (18) na wageni waishio nchini kihalali na kuwapatia vitambulisho.

Ili kutimiza lengo hilo, lengo hilo mamlaka ya vitambulisho vya Taifa itakusanya takwimu na taarifa muhimu za watu wote nchini na kuzihifadhi kwenye *data base*, takwimu hizi ndizo zitakazotumika katika kutengeneza vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, *data base* hiyo itatumiwa na wadau mbalimbali kwa utaratibu maalum ili kuhakikisha kuna usalama wa hali ya juu wa takwimu hizo, moja ya wadau ambao watumia takwimu hizi ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi, takwimu hizi zitakuwa tayari kwa matumizi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi mara baada ya *data base* hiyo kukamilika na uwishaji (*interface*) wa mifumo hii miwili yaani *data base* ya mamlaka ya vitambulisho vya Taifa na Daftari la kudumu la wapiga kura kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tulizonazo, nchi nyingi hutumia utaratibu wa kuwa na rejista ambayo wakati wa uchaguzi, mpiga kura hutakiwa kutoa kitambulisho chenye picha yake kilichotolewa na Serikali ili kuthibitisha kwamba yeye ndiye mwenye jina lililopo kwenye rejista.

Hivyo kitu cha msingi ni rejista na si *passport* au *identity card*, ndiyo maana Serikali inaandaa *data base* na vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa vitambulisho vya Taifa utasaidia sana mifumo mingine mikubwa kama daftari la kudumu la wapiga kura, taasisi za fedha, udhibiti wa watumishi hewa, kudhibiti wahamiaji haramu na hata kubaini uhalifu kwa kusaidia mambo yote haya ni matarajio ya Serikali kuwa itaokoa fedha nyingi sana.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Waziri hayakunitosheleza wala hakujibu kufuatana na niliyoyauliza, kwa kumwuuliza maswali mawili mafupi labda Bunge lako litaelewa nilikuwa na maana gani.

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza, Tume ya Uchaguzi sasa hivi inaendesha uandikishaji wa vitambulisho vya kupigia kura na ina *data base* ya kutosha kutoa *ID* za wananchi. Je, Waziri haoni ni matumizi mabaya sasa kufanya kazi ile ile upya kwa mara ya pili.

(b) Nchi hii ina matatizo ya kununua shahada za kupigia kura hasa wakati wa uchaguzi ukifika, kama tutatumia *ID* au *Passport*. Je Mheshimiwa Waziri haoni mchezo mbaya wa kununua shahada utakwisha? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza ambalo ameliuliza vitambulisho vya kupiga kura vinavyotolewa na Tume ya Uchaguzi shughuli yake ni hiyo ya kupiga kura si nyingine. Hapa tunachozungumzia ni vitambulisho vya taifa ambavyo kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri awali vitakuwa ni *multipurpose*. Kitambulisho kimoja kitakuwa na shughuli nyingi na unavyotazama kwa mwenendo huo tukiwa tumefanikisha hilo tutakuwa kwa kweli tumepunguza gharama kubwa na kitakuwa ni kitambulisho kwa kuwa zitakuwa ni teknolojia ambayo itakuwa ni vigumu sana kuweza kughushi vitambulisho hivyo. Kwa hiyo, Serikali itakuwa imenufaika katika kukata matumizi. Lakini pia hivi vitambulisho vitakwenda mbali na zaidi ya kupiga. Hivi vitambulisho vya kupiga kura ndio maana vinitwa havina tafsiri nyingine. Lakini hivi tunavyovizungumzia Mheshimiwa Ndesamburo ni vitambulisho ambavyo vitakuwa ni *multipurpose* ambavyo vitakuwa na shughuli mbalimbali na itakuwa ni vigumu sana kusema kwamba mtu anaweza akavitengeneza isipokuwa kwa teknolojia ambayo ni ya hali ya juu.

Kununua shahada nitakuwa nimelijibu katika hilo la kwanza, ni kweli kwa sababu nadhani tusingie katika suala la siasa. Maana yake kama ni suala la kununua shahada watu huuza shahada chochote kile utakachokitengeneza kama nia na madhumni ni kununua kitu kwa sababu ya kupiga kura ama kununua kura basi chochote utakachokifanya kwa sababu watu shabaha na malengo ni hayo hayo watafanya hivyo hivyo. Kwa hiyo, kwamba kama una kitambulisho hiki ama una shahada ile itazuia kuuza ama kununua nafikiri hapo ni kiasi cha kuelimisha Watanzania waelewe kwamba hayo siyo madhumuni yake. Lakini kama wana siasa madhumuni yatakuwa hayo basi hilo siwezi nikajibia. (*Makofi*)

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, mimi *concern* yangu katika suala la msingi ni (*duplication of cost*) kuongeza gharama zingine. Kama kwenye kupiga kura kuna gharama zinatumika kutengeneza *database* yake na bado kwenye vitambulisho kuna gharama tena zingine. Je, kwa nini Serikali isioanishe gharama hizi kwamba tukifanya zoezi la kuandisha wapigakura ndiyo litumike kupata *database* kwa ajili ya vitambulisho vya Watanzania? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, lengo na nia ya Serikali katika kuandaa vitambulisho vya taifa ni ku-*consolidate* mchakato mzima ambao unatumika katika kuandaa *database* mbalimbali katika kuwafahamu Watanzania na wageni ambao wako hapa nchini. *Database* ikishakamilika kama ilivyoelezwa katika jibu la msingi kutakuwa kuna *database* moja ambayo itatumika na taasisi mbalimbali katika kuwatambua Watanzania ni nani, wageni ni nani ambao wanaishi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pale tutakapokamilisha *database* ambayo inaandaliwa ni kitambulisho kimoja tu ambacho kitatumika na taasisi zote hizi na *database* itatumika situ kwa mradi wa ku-*identify* watu lakini pia katika mchakato mzima wa *registration* ya vizazi na vifo katika kufahamu watu ambao wanatakiwa kulipa kodi hapa nchini, katika kufahamu watu nani anaruhusiwa kuendesha gari na kadhalika. Hii itakuwa *consolidated effort* na itakuja kupunguza gharama. (*Makofi*)

### **Haki ya Wananchi Kumiliki Ardhi**

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI** aliuliza:-

Kwa kuwa ardhi ni mali na kwamba kila mwananchi ana haki ya kumiliki ardhi kwa utaratibu wa kiasili, kimila au kiukoo:-

Je, ni kwa nini Serikali huamua kuendeleza baadhi ya maeneo ya wananchi bila kuwapa taarifa kabla ya kuanza kazi ya uendeshaji?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Said Zafari, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa ardhi ni mali na kwamba kila mwananchi anayo haki ya kumiliki ardhi. Haki hiyo imefafanuliwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 24 (1) ambayo inatamka kuwa kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya kuhifadhi mali aliyonayo kwa mujibu wa Sheria. Aidha, haki hiyo imefafanuliwa kwenye Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 aya ya 4 ambayo imeweka wazi na msisitizo kwamba ardhi na mali ina thamani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haki ya mtu mmoja mmoja kumiliki ardhi, Serikali inayo wajibu wa kusimamia upatikanaji wa huduma na maendeleo ya watu wote, kwa mfano uwekaji wa miundombinu kama barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, njia za umeme, pia uwekaji wa huduma za jamii kama ujenzi wa shule, hospitali, pia masuala ya uwekezaji kiuchumi kama viwanda, mashamba na kadhhalika.

Kwa kuwa shughuli hizi zina umuhimu na manufaa kwa umma, Serikali huwajibika kutwaa ardhi kwa ajili hiyo. Lakini kwa kuzingatia sheria zinazohusu utwaaji wa ardhi, ikiwemo sheria ya Utwaaji Ardhi Na. 47 ya mwaka 1967 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kuwa Serikali huamua kuendeleza baadhi ya maeneo ya ardhi ya wananchi bila kutoa taarifa inayostahili. Bali Serikali inapokusudia kutwaa ardhi kwa ajili ya manufaa ya umma hufuata sheria na taratibu za nchi zilizowekwa. Kwanza, Serikali hutumia utaratibu wa kutoa matangazo kwenye maeneo husika na kwenye Gazeti la Serikali. Pili, hufanya uhamasishaji wa wananchi, hatua ya kwanza kupitia vikao na viongozi wao wakiwemo Viongozi wa Serikali za Vijiji au Mitaa, Kata, Wilaya na Mkoa na hatua ya pili, kupitia mikutano wananchi wa eneo husika.

Katika vikao hivyo wananchi wanapewa maelezo ya kina kuhusu madhumuni ya mradi, faida za utwaji wa ardhi hiyo na utaratibu mzima wa kuthamini mali zao na kulipa fidia. Kupitia vikao hivyo wananchi hupewa nafasi ya kutoa michango yao ya mawazo ambayo huzingatiwa katika utekelezaji.

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, sheria ya ardhi ya fukwe pamoja na ya ardhi ya kawaida hazina tofauti.

(a)Kama ni sawa kwa nini maelezo aliyonielea Mheshimiwa Waziri ya kwamba kupitia matangazo inapitia vikao vya wananchi hayapatikani katika Wilaya ya Kilwa katika maeneo hasa ya fukwe?

(b)Kwa nini wenye kumiliki maeneo ya fukwe katika Wilaya ya Kilwa wanapokwenda kuomba kumiliki ardhi kihalali kwa sababu wanamiliki kiukoo, kimila, wanapokwenda kuomba inakuwa ni utata mkubwa hata ule umiliki wa awali kabla ya kwenda kupata hati miliki Wizarani. Lakini wanapoomba wawekezaji inakuwa ni rahisi kupata kwa haraka zaidi? (*Makofi*)

**WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nchi kavu na kule kwenye fukwe zote zinatawaliwa na sheria hiyo hiyo moja. Sasa taarifa kwamba kule Kilwa sheria ya ardhi haifutwi ndiyo naisikia sasa hivi kwa kama anayo mifano ambayo kule Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imechukua maeneo bila kufuata sheria hii basi Mheshimiwa Mbunge leta taarifa Wizarani kwangu na ninaahidi kwamba tutafuatilia kwa sababu sheria ni moja kwa nchi nzima. (*Makofi*)

La pili, kuhusu umilikishwaji wa ardhi katika maeneo ya fukwe kwamba wananchi hawamilikishwi lakini wawekezaji wanamilikishwa haraka haraka. Wananchi kule Kilwa kama ilivyo wawekezaji hatua ya kwanza ukitaka kumilikishwa eneo inanzia kule kule kwenye Halmashauri ndiyo hatua ya kwanza vikao vinakaa kule kule. Serikali ya vijiji siyo Serikali sheria inasema *village assembly* maana yake ni kijiji chote.

Mkutano wa kijiji ndiyo kikao cha kwanza kinachosema kwamba fulani amilikishwe hapa ni eneo lake tunathibitisha amilikishwe au huyu mwekezaji amilikishwe ni kikao cha kwanza. Kikao cha pili ni ngazi ya Halmashauri na sisi Wizarani pale huwa tunahitimisha tu. Huo ndiyo utaratibu wa kufuatwa na naomba na Kilwa wafuate utaratibu huu.

**MHE. MAGADLENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa sheria inasema kwamba vikao vianzie kwenye ngazi za vijiji kwa wananchi ambapo ndiyo wenye ardhi lakini utaratibu unaofanyika ni kwamba wawekezaji wanapotaka eneo kwa ajili ya kuwekeza wanaanza kwenye ngazi ya Serikali Kuu na hivyo wanafika kule wakiwa na vibali tayari. Na hata pale wananchi wanapotoa maoni yao hayasikilizwi kwa sababu tayari yule mtu anakuja na jeuri ana kibali na pengine hata watu wameshawekwa sawa kwenye ngazi za juu. Tumeona maeneo mengi kwa mfano shamba la Mbarali

wananchi walilalamika sana lakini lilitolewa kwa nguvu na sasa hivi tumeona matokeo yake hakuna kinachofanyika, tumeona maeneo ya *Gulmeti Game Reserve* wananchi wamelalamika sana mpaka sasa wananyanyasika. Kuna maeneo ya fukwe mbalimbali ambapo bado ni kero wananchi hawasilizwi kwa sababu wawekezaji wanaanzia juu. Serikali inasema nini kuhusiana na hili? (*Makofi*)

**WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa nisikubaliane naye kabisa kabisa kwamba anayeomba kumilikishwa ardhi anaanzia Serikali Kuu si kweli hata kidogo kwa sababu sheria iko wazi kabisa kwamba anayeomba kumilikishwa ardhi mwekezaji lazima aanzie kwenye kijiji na kikao cha kwanza ni *village assembly*. Yaani kikao kina wanakijiji wote hiyo ndiyo sheria na ndiyo tunayofuata. Shamba la Mbarali ni mfano mbaya kwa sababu yale yalikuwa ni mashamba ya Serikali yalikuwa mashamba ya *NAFCO* mfano mbaya hauhusiani na ardhi ya kijiji. Napenda kuwahakikishia Watanzania popote pale walipo kwamba mwekezaji yeyote anayetaka ardhi wao ndiyo wa kwanza kujadili jambo hili ndiyo wenye ardhi. (*Makofi*)

Na. 10

### **Shirikisho la Afrika Mashariki**

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inalenga katika kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki na hatimaye kuwa na Rais wa Shirikisho.

(a) Je, lengo hilo litakapokamilika kutakuwa hakuna nchi za Uganda, Kenya, Tanzania, Rwanda na Burundi kama ilivyotokea kwa nchi za Zanzibar na Tanganyika, baada ya kuundwa Tanzania?

(b) Je, kama jibu ni ndiyo au hapana utaratibu wa shirikisho hilo utakuwa vipi?

**NAIBU WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki, ni hatua ya mwisho katika mtangamano wa ushirikiano. Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeainisha hatua nne za mtangamano ambazo ni Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Sarafu moja na hatua ya mwisho ni shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Hatua ya kwanza yaani Umoja wa Forodha ilianza kutekelezwa Januari, 2005 baada ya itifaki yake kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Hatua ya pili ya soko la pamoja iko katika mchakato wa majadiliano. Hatua nyingine za ushirikiano zitafuata kwa kuzingatia matokeo ya utekelezaji wa hatua ya

kwanza na ya pili na mashauriano miongoni mwa nchi wanachama ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa wananchi pamoja na Mabunge ya Nchi wanachama. Baada ya maelezo haya napenda sasa kumjibu Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, maswali yake yenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki, bado halijafikiwa. Kutokana na mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi wanachama zinatakiwa kuwa na mazungumzo ya pamoja ili kufikia itifaki ya utekelezaji wa hatua yoyote ya ushirikiano. Wakati muafaka wa kuanzisha Shirikisho la Afrika Mashariki ukifika mchakato wa mazungumzo ya itifaki ya Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki utaanza na mchakato huo ndio utakaoamua aina ya shirikisho na muundo kwa kuzingatia maoni ya wananchi. Kutokana na hali hiyo kwa sasa itakuwa vigumu kumweleza Mheshimiwa Mbunge aina ya muundo wa shirikisho mpaka pale tutakapofikia hatua ya nne ya mtengamano na wananchi kuamua aina ya shirikisho watakaloona linafaa.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba sasa hivi tuko katika mchakato wa majadiliano wa sehemu ya pili ya shirikisho la Afrika Mashariki. Lakini wakati huo huo Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi za *COMESA* na *SADC* nazo ziko katika mchakato wa kutafuta soko la pamoja.

Je, katika hali hii, hii Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa na mazungumzo gani au itakuwa namna gani katika kujiunga na hili Shirika la *COMESA* na *SADC* ambalo sasa hivi wanatafuta njia ya kuwa na soko la pamoja katika hali hii ngumu ya uchumi katika duniani? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kama jibu langu la msingi nilivyoeleza kwamba hatua yoyote inayofikia ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inahitaji mazungumzo ya awali baina ya nchi zote wanachama. Na ni hatua hiyo hiyo itakayopelekea kwamba pale tutakapoamua kwa pamoja kuwa na mashirikiano yoyote yote kati yetu, *COMESA* na *SADC* basi utakuwa ni uamuzi wa pamoja wa nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wakuu wetu wa nchi wameshatoa maelekezo kazi iliyobakia ni ngazi zinazofuata kwa mashirikiano kuanza mazungumzo ya namna itavyofaa kwa kuwa na umoja ulio mkubwa zaidi wa soko la pamoja na kufanya biashara kwa pamoja.

Na. 11

### **Tatizo la Wanafunzi Kupata Mimba**

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inasisitiza kuwa watoto wa kike wapewe fursa kubwa ya kusoma na kwa kuwa hivi karibuni kuna wimbi kubwa la wasichana hao kupata mimba hasa wale wa shule za msingi:-



- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani katika kuzuia tatizo hilo?
- (b) Je, mpaka sasa ni wanafunzi wangapi wamepata tatizo hilo na mikoa gani inaongoza:-

**NAIBU WAZIRI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maulidah Anna Komu Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa wapo wanafunzi wa shule za msingi wanaopata mimba. Ili kuzuia tatizo hilo Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

- Kuhamasisha jamii ili kusimamia uendeshaji madhubuti wa shule kupitia kamati hai za shule.
- Kuelimisha wazazi, walezi jamii na wanafunzi ili kuepukana na vitendo vinavyochangia wanafunzi kupata mimba.
- Kuweka kanuni inayotoa adhabu kali kwa wanaume wanaowapa mimba wanafunzi. Adhabu hizo ni kifungo cha muda mrefu kisichopungua miaka 30 na kufukuzwa kazi. na utumishi kwa walimu wanaobainika kuhusika na mimba za wanafunzi hao.
- Kwa kuwa utalaam wa kipima vinasaba (*DNA*) sasa upo Serikali imeazimia kutumia kipimo cha *DNA* ili kuthibitisha waliohusika na kuwapa wanafunzi mimba.

(b) Mheshimiwa Spika, wanafunzi waliopata mimba kwa mwaka 2006/2007 (hadi Juni 2007) ni 3,195 sawa na asilimia 6.0 ya wanafunzi wote walioacha shule kwa kipindi hicho. Aidha, Mikoa iliongoza ni Mtwara (435), Mwanza 306, Tanga 290, Morogoro 281, Ruvuma 204 na Lindi 144. Ahsante.

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilitoa kauli kuwa watoto wa kike waachwe wasome mara wanapopata mimba. Na kwa kuwa kauli hiyo pia iliwekewa msisitizo mkali sana na Mheshimiwa Rais wetu.

(a) Je, mpaka sasa Serikali imejipangaje kuwasaidia wale ambao tayari wameshaathirika na tatizo hilo ili waweze kurudi na kuendelea na masomo yao?

(b) Kwa vile nchi yetu bado imekumbwa na janga kubwa sana la rushwa. Je, hivi vipimo vya *DNA* Serikali inajua kwamba vinaweza vikabadilishwa, wamejiwekaje kwa tatizo hilo litakapokuja kutokea? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais amehamasisha sana tukishirikiana na Wabunge kwamba mtoto wa kike ache asome na mimi naomba kuungana naye kwa niaba ya Waziri wangu kwamba sisi Wabunge tuchukue nafasi hiyo kwanza maana ni wawakilishi wa wananchi kila Mbunge kwenye nafasi yake akemee kwa sababu wanaowapa mimba ni watoto wa kiume wetu au wa ndugu zetu au wa jirani zetu.

Lakini pia tunayo nafasi kubwa ya kuhamasisha juu ya malezi ya mtoto wa kike. Turudie maadili siyo kila mila za zamani ni mbaya kwa hiyo, tuwatumze watoto wa kike. Serikali imejipanga kutoa elimu ya uzazi na inatolewa pamoja na kueleza athari na kwamba itawakatisha katika malengo na mipango yao.

Suala la kuwarudisha ni suala ambalo tunasubiri sera inayoboreshwa, hivi sasa tunapokea maoni ya wadau mbalimbali, baada ya kumaliza mchakato wa sera ndipo tutakapona sera imetuelekeza nini na sheria itatengenezwa ya kuweza kujua nini kifanyike ama kuwarudisha ama kutowarudisha.

Hata hivyo itabidi pia tushirikiane na wenzetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa karibu kwa sababu tunaweza tukagongana katika utekelezaji wa kazi zetu. Wenzetu wanahimiza sana afya ya mama na mtoto. Sasa sisi tutapoamua arudi mtoto atabaki wapi atalelewa na nani na mambo mengine. Kwa hiyo, naomba tusembiri sera itakavyotuelekeza.

Kuhusu kipimo cha kinasaba naomba nimhakikishie kwamba dhamira ya Serikali ni kuwasaidia hawa watoto wa kike lakini pia kuweza kuwabaini wale majadume mabazazi ambao kazi yao kuwapa watoto mimba na kuwakimbia.

Sasa akikataa yeye hata shati lake tukiona tumeshindwa tutachukua hata hatua zaidi. Naomba atumiani tuko na dhamira njema, sote tunajenga nyumba moja tusaidiane. (*Makofi*)

Na. 12

### **Tofauti ya Uendeshaji wa Shule za Serikali na Binafsi**

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI** atauliza:-

Kwa kuwa hapa nchini kuna shule za Serikali na zile za binafsi (*Private*):-

(a) Je, Serikali inasimamia silabasi na mitaala ya shule hizo kwa pamoja?

(b) Je, mitaala na silabasi zinazotumika zinafanana?

(c) Je, shule za binafsi zinatumia mitihani ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) (b) na (c) naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Shule za binafsi zimegawanyika katika makundi matatu ambayo ni:-

(i) Shule zinazofundisha mtaala wa Tanzania kwa kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia kuanza chekechea hadi darasa la saba na Kingereza katika shule za sekondari, vyuo na vyuo vikuu.

(ii) Shule zinazofundisha mtaala wa Tanzania kwa kutumia lugha ya Kingereza kufundishia kuanza elimu ya chekechea na msingi. Shule hizi hufahamika kama (*English Medium Schools*).

(iii) Shule za kimataifa ambazo hutumia mtaala unaotambulika kimataifa. Shule hizi hufahamika kama (*International Schools*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Zulekha kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali husimamia silabasi na mitaala ya shule za serikali na zisizo na Serikali kwa pamoja. Aidha, shule zote hukaguliwa na wakaguzi wa shule wa Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, mitaala inayotumika katika shule binafsi zinazotumia lugha ya Kingereza (*English Medium Schools*) kufundishia hufanana na mitalaa inayotumika katika shule za Serikali. (Makofi)

*International Schools* hutumia mitaala tofauti na mitihani yake hutungwa na taasisi husika za Kimataifa kama vile *University of Cambridge Local Examination Syndicate* na *International General Certificate of Secondary Education*.

(c)Mheshimiwa Spika, shule za binafsi zinazotumia mitaala ya Serikali hufanya mitihani inayotungwa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Mitihani hiyo ni sawa na ile inayotumiwa na Shule za Serikali tofauti yao ni lugha.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, je, kama mwanafunzi alisoma shule ya *international* sasa anaweza kubadilisha asifanye mtihani ule wa *international* afanye mtihani wa Serikali inawezekana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, mwanafunzi ambaye anasoma katika shule ya *international* atakapokuwa anataka kufanya mtihani wa Serikali anaweza anaruhusiwa. Anachopaswa kufanya ni kutoa taarifa kabla ya muda wa usajili katika Baraza la Mitihani haujakamilika. Ahsante.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba *curriculum* na *syllabus* kwa shule za *private* na za *public* ukiondoa zile za *international school* zinafanana.

Kama hivyo ndiyo Mheshimiwa Waziri anaweza kunipa sababu ni kwa nini shule hizi za *private* hususan zile zinazoongozwa na mashirika ya kidini, kila mara katika mitihani ya kidato cha nne wanakuwa wakiongoza na kuzizidi hata zile shule tunazoziita *special schools* kama Kibaha, Mzumbe, Kilakala na nyinginezo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mitihani hutungwa na Baraza la Mitihani, *syllabus* wanayotumia na mitaala inafanana tofauti ni lugha za kufundishia kwa maana hizi ambazo ni *English Medium* hutumia lugha ya Kingereza.

Hata hivyo zipo shule si zote kwamba kila siku shule zote za *private* hufanya vizuri. Naomba nikuhakikishie kwamba shule zetu za Serikali hufanya vizuri pamoja na kwamba hizi ambazo ni maalum zinaweza zisifikie kwenye kiwango kilichotarajiwa.

Naomba tusiwakatishe tamaa wale ambao wako kwenye shule za Serikali. Wanasoma vizuri, katika mazingira ambayo Serikali yao imewawezesha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea nilikuwa napenda nimpongeze Naibu Waziri wa Elimu Mheshimiwa Mahiza juzi alifanya kitu ambacho mimi kinanivutia sana, nacho ni kwamba kulikuwa na tatizo la wanafunzi, badala ya kupiga mbizi alikwenda kukabiliana nalo ana kwa ana.

Nadhani nawafahamu baadhi ya viongozi kunapokuwa na tatizo wanapiga mbizi ndiyo tabu. (*Makofi*)

**Sifa za Kuteuliwa Mtendaji Mkuu wa Jeshi**

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jeshi la Wananchi linaendelea kukua na kuimarika kivita na kiukombozi:-

Je, ni sifa gani zinazohitajika kielimu, uzoefu wa kazi, nidhamu au vigezo vingine kwa Rais kuteua watendaji katika nyadhifa za Mkuu wa Majeshi (*CDF*), Mkuu wa Mafunzo na Utendaji Kivita (*COT*), Mnadhimu Mkuu (*Chief of Staff*) na Mkuu wa Wafanyakazi (*CP*).

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya kuwateua watendaji wakuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika nyadhifa za Mkuu wa Majeshi (*CDF*), Mnadhimu Mkuu (*Chief of Staff*), Wakuu wa Fomesheni na Vikosi, ni ya Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Kwa mujibu wa Katiba – Sura, Ibara 148(2) (a) na Sheria ya Ulinzi wa Taifa, 2000, sehemu ya pili, Ibara 15(1) na 16(1). Aidha katika kufanya uteuzi huo Rais halazimiki kufuata vigezo vyovyote.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa kuwa Jeshi ni taaluma, sifa za maendeleo ya utumishi kama vile kiwango cha elimu ya jumla, elimu ya kijeshi, tabia na mwenendo (hasa nidhamu na uadilifu), uwezo wa uongozi wa kijeshi, uwezo wa kumudu madaraka na uwezo wa kuwafunza wafuasi ni vigezo muhimu kwa Viongozi Wakuu wa Kijeshi.

Maafisa Wakuu wa Jeshi hupata fursa kufanya kozi za viongozi kama kozi ya Ukamanda na Unadhimu (*Command and Staff Course*), kozi ya ulinzi kwa Makamanda wa Juu (*High Commanders Defence Studies*), kozi ya Vita (*War Course*) na kozi ya Ulinzi wa Taifa (*National Defence Course*).

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa sina pingamizi na ibara ya 148 (2); na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Rais halazimiki kufuata vigezo vyovyote; je, kwa nini sasa kwa muda wa miaka 44 ya Muungano hakuna mtu yeyote kutoka upande mwingine wa Muungano, nikimaanisha Zanzibar,

aliyechaguliwa katika vyuo hivyo ukiacha mmoja aliye-act kwa muda wa miezi na baadaye akahamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa?

Kwa kuwa katika jibu lake Waziri amekiri pia kwamba elimu ni kigezo muhimu na jeshi ni taaluma; je, anakusudia kuniambia kwamba kwa upande mwingine wa Muungano, elimu kama hii au mafunzo kama haya hayajatolewa ndiyo maana hajachaguliwa mtu kama huyo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kweli kwamba, kwa miaka 44 hajatokea Mkuu wa Majeshi kutoka Zanzibar, lakini Mkuu wa Nchi au Amiri Jeshi Mkuu, haangalii mtu anatoka wapi; anaangalia sifa na uwezo.

Katika sifa na uwezo, Mkuu wa Nchi aliangalia waliopatikana ni hao waliopatikana, labda nimhakikishie tu, kadiri atakapopatikana mwenye sifa na Mheshimiwa Rais bila kusita atamchagua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sifa nyingine alizozielezea Mheshimiwa Mnyaa za elimu, nakuhakikishia kwamba, wapo wenye sifa za elimu Zanzibar na waliopo kwenye nafasi mbalimbali za uongozi wanafanya kazi zao vizuri.

Na. 14

### **NSSF Kuendeleza Miradi Mbalimbali**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ilipendekeza kuwa NSSF inaendelea kujenga majengo kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwemo kuboresha biashara za Wamachinga katika Mji wa Arusha na Mwanza: Je, ushauri huo kwa NSSF umepokewaje na wafanyabiashara (Machinga) wa Mwanza ambao tayari wapo katika maeneo yanayoeleweka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kazi, tunakukaribisha sana ni muda mrefu umekuwa katika kuuguza afya yako, natumaini umerudi na afya njema.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naendelea vizuri, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *NSSF* imekwisha wasiliana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza, pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Arusha kuomba maeneo ya ujenzi wa majengo yatakayotumiwa na wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama Wamachinga.

Tayari Halmashauri ya Jiji la Mwanza, imekwishatenga eneo lililopo Mlango Mmoja, lenye ukubwa wa ekari moja na nusu kwa ajili ya mradi huo na wataalam wa *NSSF* wametembelea na kuridhika nalo. Halmashauri ya Jiji la Mwanza imepanga kutuma wataalam wake Dar es Salaam ili kujifunza utaratibu mzima uliotumika katika kupanga na kutekeleza Mradi wa Jengo la Wamachinga, linalojengwa Wilaya ya Ilala. Baada ya hapo, Halmashauri ya Jiji la Mwanza itawasilisha rasmi pendekezo la Mradi kwa *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Arusha, shirika linasubiri Halmashauri ipate kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wafanyabiashara ndogo ndogo ili hatua nyingine za utekelezaji wa Mradi huu zifuate.

Mheshimiwa Spika, ingawa Wizara haijafanya utafiti kuhusu maoni ya Wamachinga ni matarajio yetu kuwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, ambayo inasimamia mipango ya maendeleo kwa niaba ya Wananchi wa Mwanza, itakuwa imezingatia matakwa yao wakati wa kuleta maombi rasmi ya Mradi huu.

Hata hivyo, kwa kuwa ushauri huu uliotolewa wa kutenga na kujenga maeneo ya biashara, unalenga kuwaendeleza na kuwaondolea bugudha wafanyabiashara wadogo wadogo (Wamachinga). Matarajio ya Serikali ni kuwa miradi hii katika Mji wa Mwanza na Arusha, itapokelewa vizuri na kuungwa mkono kama ilivyo kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Naibu Waziri amesema kwamba, tayari Mwanza imetenga eneo la Mlango Mmoja na kwamba Halmashauri imejipanga kwenda kuchukua mafunzo Ilala, Dar es Salaam. Je, yupo tayari sasa kutoa maendeleo ya hatua hizi mbili ili hawa wafanyabiashara wadogo wadogo wajue Serikali imefikia hatua gani?

Kama Serikali itapendezwa na mwenendo mzuri wa kuupokea Mradi huu Mwanza kwa kuanzia na Mlango Mmoja; je, inaweza ikaruhusu pia tukaendelea basi Mwanza na maeneo mengine kama Kiloreli, Nyakato Sokoni na mengine ili kukidhi hitaji na Wamachinga hawa kuweza kupata maeneo bora ya biashara zao?

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Naibu Waziri hujajibu, nimeghafirika kidogo muda wa maswali umepita. Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, tumeanza na shughuli ya kumwapisha mwenzetu na ilichukua muda kidogo na ndiyo maana navuta tuyamalize haya maswali, limebaki moja tu. Kwa hiyo, majibu kwa swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:**  
Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, kwa kweli Watendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, wameahidi kuja kujifunza Dar es Salaam pale Ilala ili Mradi huu uendelee.

Mimi ningependa kutoa wito kwa Wabunge wa Mwanza, tushirikiane kuhamasisha hatua hizi ziende kwa haraka, kama Watendaji hawajawa tayari kuja basi sisi kama Wabunge ambao tunaona umuhimu wa masuala haya na umuhimu kwa Wamachinga kuwa na biashara hizi, basi tuhakikishe kwamba, hatua hizo zinafuatwa kwa sababu hatua zilizopo sasa zipo kule Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

Kuhusu suala la pili la maeneo mengine, mimi nadhani ni wazo zuri kabisa, itategemea tu kama ile *visibility study* itakuwa imekubalika fedha zitapatikana *NSSF* au eneo lingine. Si lazima *NSSF* ijenge kwenye maeneo hayo, kama kuna wawekezaji wengine, mimi nadhani ni jambo zuri kuwa na maeneo zaidi ya Mlango Mmoja pekee.

Na. 15

### **Ukosefu wa Ajira na Kufungwa kwa Vijana Magereza**

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa idadi kubwa ya vijana katika magereza ni wale wenye makosa yanayotokana na uhalifu kama vile wizi; na kwa kuwa hali hiyo huchangiwa na ukosefu wa ajira:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa kwa kuboresha magereza inawavutia vijana wengi kupenda kuishi gerezani kulikoni uraiani?
- (b) Je, Serikali inayo mikakati gani mahususi kwa vijana kupata ajira hasa wale wa elimu ya msingi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, vijana kama raia wengine wa Tanzania, wanatakiwa kupewa mahitaji muhimu anayotakiwa kupewa binadamu hata wanapokuwa gerezani. Mahitaji haya muhimu ni pamoja na maji safi, chakula bora na malazi safi. Kwa muda mrefu, wafungwa wengi wamekuwa wakipata huduma duni ingawa ni haki yao kupata huduma bora licha ya kuwa ni wafungwa.



Suala la kuboresha magereza ni mpango wa kuwapatia maisha bora wananchi wake wakiwemo wafungwa vijana. Magereza yanatakiwa kuwa mahali ambapo vijana watapata ujuzi na stadi za kazi zitakazowasaidia hata baada ya kumaliza vifungo vyao. Aidha, Serikali itaendelea kuwaelimisha vijana walioko magerezani, umuhimu wa kuishi kama raia wema uraiiani kuliko kuvutiwa kuishi gerezani.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu mikakati mahususi ya Serikali kwa vijana kupata ajira hasa wa shule za msingi, kutokana na uchache wa nafasi za ajira katika sekta iliyo rasmi, Serikali inawahamasisha vijana wengi wanaomaliza shule za msingi, kujiunga katika vikundi vidogo vidogo vya uzalishaji mali ili waanzishe miradi ya uzalishaji mali kwa nia ya kujipatia kipato.

Katika kuwasaidia vijana hawa, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, hutoa mafunzo ya ujasiriamali, uongozi, uanzishaji, uendelezaji na usimamizi wa miradi ya uzalishaji mali. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya, Serikali hutenga maeneo ya kufanyia kazi, kilimo na ufugaji wa vijana.

Kupitia Mfuko wa Uwezesaji wa Maendeleo ya Vijana na Taasisi nyingine za Fedha, Serikali hutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kuwasaidia vijana na vikundi vilivyoamua kujiajiri, kupata mitaji itakayowasaidia kuimarisha biashara zao.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Naipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi nzuri ambayo imeendelea kuboresha hasa wafungwa wetu, kwa maana ya kupata chakula, maji safi, pamoja na malazi.

Waziri anakubaliana na mimi kwamba sasa wananchi au vijana wanafurahia kukaa magerezani kuliko kukaa uraiiani kwa sababu ya ugumu wa maisha ukilinganisha kwamba magereza yameboreshwa kuliko wananchi wanavyoishi?

Wizara ya Mambo ya Ndani imejipanga vipi kuhakikisha kwamba vijana wanapokuwa kule magerezani wanaweza kupata mafunzo ambayo yatawasaidia pindi watokapo magerezani waweze kuwa na utaalumu utakaowasaidia kuendesha maisha kuliko kuingia kule na hatimaye wanatoka pasipo kupata ujuzi wowote?

**SPIKA:** Nadhani linaelekezwa zaidi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuliko Wizara ya Kazi, kwa hiyo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kusema kwamba, sera ya kuendelea kuboresha magereza yetu tutaendelea nayo, kwa sababu vijana wetu ambao wapo ndani ya magereza, wana haki ya kuishi kama binadamu. Hiyo kazi tutaendelea kuifanya, lakini pia Serikali yetu itajitahidi kuendelea na sera ya kuboresha maisha ya kila Mtanzania; waliopo magerezani na ambao wapo nje ya magereza.

Mheshimiwa Spika, Sera Kuu ya Wizara ya Mambo ya Ndani katika magereza yetu ni urekebishaji wa tabia ya wafungwa. Katika kazi hiyo ya kurekebisha tabia ya

wafungwa, tutaendelea kuwasomesha kwa kutumia taasisi kama VETA na kadhalika ili kuhakikisha kwamba, vijana ambao wapo magerezani, wanatoka na ujuzi na tabia nzuri zaidi ili waweze kuishi maisha bora wakiwa nje ya magereza yetu. (*Makofi*)

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wanapokuwa magerezani hupata mafunzo; je, kwa nini Serikali isiwape mafunzo vijana uraiani kabla hawajaingia ili wasiweze kuingia jela kwa sababu wanakuwa *idle*; kwa kuwa hawakupewa elimu ndiyo maana wanaingia katika matendo ya uharifu wanayoyafanya wafungwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba tunangojea vijana waende magerezani ndiyo tuwape mafunzo. Mafunzo yamekuwa yakitolewa kwa vijana wengi tu, kwanza vijana waliopo magerezani ni wachache sana ukilinganisha na vijana waliopo nje, ambao tumepanga mikakati mingi sana ya kuwapa mafunzo hasa ya stadi ili waweze kujitegemea kwa kujiingiza katika shughuli za kiuchumi.

Tunasema kwa wale ambao kwa bahati mbaya wanaingia gereza, basi huko huko magerezani tunaendelea na mafunzo kama haya ambayo yanatolewa ili wakitoka waendeleo kuwa na stadi ambazo zitawawezesha kujitegemea na kujipatia vipato vyao. Kwa hiyo, nilitaka niseme tu kwamba, mafunzo hutolewa kwa wingi zaidi kwa vijana waliopo mitaani na hata magerezani tunatoa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita kidogo. Matangazo na kama kawaida naanza na wageni; wageni wa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Naibu Kiongozi wa Upinzani Bungeni ni wafuatao; nadhani wengi wamekuja kwa tukio la kuapishwa kwa Mbunge mpya ambaye anatoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA); naomba tutambue kuwepo Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mwenyekiti Taifa wa CHADEMA. Karibu sana Mheshimiwa, ila ninakusihii unapokwenda Urambo usiwe unatoa maneno makali sana. (*Kicheko*)

Wengine ni kama ifuatavyo; ni familia ya Mheshimiwa Charles Mwera, wengi ni akina Mwera; kuna mmoja anaitwa Mzee Mwera, nadhani atakuwa ama ni baba yake au ni mjomba, ndiyo baba mzazi karibu sana baba. (*Makofi*)

Yupo Ndugu Peter Mwera, nadhani naye ni sehemu ya ukoo, wanafuata Prisca Mwera, Esther Mwera, hatujaambiwa hawa ni dada zake au wakeze, lakini mnakaribishwa sana. Denis Mwera, Loyce Mwera, huyu Mheshimiwa ana ukoo mpana sana labda ndiyo unamsaidia hata kwenye kura nadhani, Nyanguru Mwera, Godfrey Mwera halafu wanafuata wengi tu wengine ambao amefuatana nao, sehemu ya familia sitaweza kuwataja wote ni wengi karibuni sana.

Wapo Madiwani toka Jimbo la Tarime kama ifuatavyo: Mheshimiwa Abel Mchele huyu ni Diwani wa Kata ya Nyamwaga, Mheshimiwa Joseph Mcherenya Kata ya Mwema, Mheshimiwa Abdul Maswi, Kata ya Nyarero, Mheshimiwa Thecla Johanes, Diwani wa Viti Maalum Tarime, Mheshimiwa Mary Nyagabona, Diwani wa Viti Maalum, Mheshimiwa Magreth Sang'au, Diwani wa Viti Maalum na Mheshimiwa Gati Nyerere, Diwani wa Viti Maalum. Wewe Nyerere upo CHADEMA? (*Kicheko*)

Wengine ni Dr. Kapwani, Mwenyekiti wa Mkoa wa Iringa CHADEMA, yupo Ndugu John Mrema na Mkurugenzi, Kurugenzi ya Bunge na Halmashauri CHADEMA, Ndugu Chacha Ukong'o, Afisa wa CHADEMA Mkoa wa Mara, Bi. Suzan Kiwanga, Afisa wa CHADEMA, Ndugu Omar Chitanda, Afisa Mwandamizi Kurugenzi ya Sheria na Katiba CHADEMA, Bi. Stella Masanja, Afisa wa CHADEMA na wengine; Karume Jeremiah Ngunda, naomba wale vijana 21 waliomsindikiza Mheshimiwa Charles Mwera kutoka Tarime nao wasimame. (*Makofi*)

Ila *Sergeant-At-Arms* hamkumwona, naona kama amevaa sare ya CHADEMA hivi; nadhani hii hairuhusiwi. Hatuvai sare za vyama vyetu humu ndani, lakini basi wote mliokuja karibuni sana tuketi, ahsante sana.

Kwa kauli hiyo, napenda kumkaribisha kwa niaba yenu Mheshimiwa Charles Mwera, karibu sana Bungeni, natumaini utatoa mchango wako vizuri, kwa uzalendo na bila jazba. Wapo wageni wa Mheshimiwa Pindi Chana ambao ni Ndugu Damian Ndelwa, Ndugu Emmanuel Swai na Mama Benedict Michael.

Mgeni wa Mheshimiwa Martha Mlata ni Frank Mkinza kutoka London Uingereza, yeye ni Mwenyekiti wa CCM Shina la Hilington London. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Godfrey Zambi ambaye ni Bwana Ben Mwambasi anaishi Dar es Salaam ni mdogo wake Mheshimiwa.

Wageni wa Kamati ya Bunge ya UKIMWI ni Mheshimiwa Catherine Buburia, aliyewahi kuwa Senator katika Bunge la Highland. *You are warmly welcome. We are very happy that you have been able to find time to join us here in Dodoma and continue with great work in fighting HIV/AIDS.* Amefuatana na Frank Kaitale, Afisa Mradi wa OVS. Karibuni sana wapambanaji dhidi ya UKIMWI.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wanamichezo 11 wa michezo ya SHIMISEMITA Kitaifa kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, wakiongozwa na Bi. Elizabeth Kingaraza, nadhani hawa ni wageni wa Mheshimiwa Azan.

Matangazo ya kazi zetu; Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, ameniomba niwatangazie kuwa leo tarehe 28 Oktoba, 2008 saa 05.30 asubuhi, kutakuwa na Kikao Maalum cha kuzungumzia mabadiliko ya Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi wa Mwaka 2008. Kikao hicho kitafanyika Ukumbi Na. 231, ghorofa ya pili katika Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anatangaza kwamba, kutakuwa na kikao cha Kamati yake hiyo katika Ukumbi Na. 227 kuanzia saa tano asubuhi.

Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo, wakutane mara baada ya kipindi cha maswali ili waonane na Mjumbe wa Baraza la AWEPA, yule mgeni kutoka Highland niliyemtambulisha awali.

Waheshimiwa Wabunge, Kiongozi wa Shughuli za Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, bado yupo India kwa matibabu. Pia nimepata waraka mfupi wa Mheshimiwa Dr. Slaa, Naibu Kiongozi wa Upinzani kwamba, naye ana shughuli kule Jimboni Karatu, kwa hiyo ameniarifu kwamba, anayeshikiria au kukaimu Uongozi wa Kambi ya Upinzani kwa muda huu hadi wakubwa watakaporudi ni Mheshimiwa Khalifa. Namtakia mema katika shughuli hizi ambazo atazifanya kwa siku moja, mbili au tatu; basi vyovyote vile hayo yatakuwa ni mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho, kwa shingo upande, napenda kuipongeza Timu ya Yanga kwa ushindi wake dhidi ya Simba. Nasema kwa shingo upande, kwa sababu ushindi wenyewe umegubikwa na utata wa kila namna.

Sasa ingawa wao wanashangilia, lakini ushindi wa namna hii tunataka goli safi, wazi, sasa mara kadi nyekundu tatu, mara hirizi zinafichwa kwenye magoli!

Mheshimiwa Waziri Mkuchika, angalia mambo haya, matumizi ya fedha nyingi sana ambazo hatuelewi zinatoka wapi.

Baada ya kusema hayo, nina udhuru, naomba Naibu Spika aendelee na shughuli zilizobaki.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Asalaam Alaykum? Watu wote wakishindwa watasema kuna sababu, haya tunaendelea. *(Makofi)*

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Usajili wa Makandarasi wa Mwaka 2008 *(The Contractors Registration (Amendment) Bill, 2008)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kisha lipitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya *The*

*Contractors Registration Amendment Act, 2008*, pamoja na jedwali la marekebisho, kama ilivyotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kufanya marekebisho katika Sheria Na. 17 ya Usajili wa Makandarasi ya Mwaka 1997, inayotumika hivi sasa ili kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Bodi na hivyo kuiwezesha Bodi kufanya kazi kwa ubora na ufanisi.

Aidha, kutokana na mabadiliko mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kupitishwa kwa Sera ya Ujenzi ya Mwaka 2003, kupanuka na kukua kwa haraka kwa Sekta ya Ujenzi na kuwepo kwa taasisi zenye mamlaka yanayokaribiana au kushabihiana na yale ya Bodi. Sheria hiyo imeonekana kuwa na upungufu sana, hali inayosababisha Bodi kukosa uwezo wa kisheria katika usimamizi, uratibu na udhibiti wa shughuli za kikandarasi nchini. Kabla ya kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu marekebisho ya vifungu vya Muswada huu, naomba nitoe maelezo kwa kifupi kuhusu upungufu uliopo katika Sheria ya sasa kama ifuatavyo:-

Moja, Sheria ya sasa ina makosa mengi ya uchapishaji na vilevile ina vipengele ambavyo ama vinajirudia au vinapingana. Upungufu huu umesababisha Sheria hii kutoeleweka vizuri.

Mbili, Baadhi ya majukumu ya Bodi yameandikwa kiujumla na hivyo kuleta utata katika utekelezaji wa sheria kwa ufanisi. Aidha, kukosekana kwa vipengele vya kuipa Bodi uwezo wa kisheria kuhoji ubora wa kazi za makandarasi waliosajiliwa kama njia ya udhibiti wa kazi za kikandarasi, kunapotosha malengo ya kuwepo kwa sheria yenyewe.

Tatu, Sheria ya sasa haina uwezo wa kusimamisha mradi au shughuli yoyote ile ya kikandarasi, ambayo itafanyika bila kuzingatia matakwa ya sheria, hususan pale usalama wa watu na mali zao unapokuwa hatarini.

Nne, Sheria ya sasa haitamki bayana ni kwa kiasi gani watu binafsi wanapovunja sheria hii wanaweza kuchukuliwa hatua. Matokeo yake ni kwamba, zaidi ya watu binafsi 12 waliofikishwa mahakamani katika kipindi cha mwaka 2003 - 2008 kwa kosa la kufanya kazi ama kuruhusu majengo yao kujengwa na watu wasio makandarasi waliosajiliwa, wameachiwa huru na Mahakama kwa maelezo ya kuwa Sheria ya sasa inahusu Wakandarasi pekee.

Matokeo yake ni kwamba, zaidi ya watu binafsi 12 waliofikishwa mahakamani katika kipindi cha mwaka 2003 – 2008 kwa kosa la kufanya kazi ama kuruhusu majengo yao kujengwa na watu wasio Wakandarasi waliosajiliwa, wameachiwa huru na Mahakama kwa maelezo ya kuwa Sheria ya sasa inahusu Wakandarasi pekee. Upungufu huu wa kisheria, unaifanya Bodi kukosa nguvu za kusimamia Sheria hasa kwa watu binafsi na hivyo kuendelea kuhatarisha usalama wa watu na mali zao kwa kuwa wameendelea na kazi za ujenzi pasipo kutumia huduma za Wakandarasi.

Tano, Sheria ya sasa haiipi Bodi nguvu za Kisheria za kuwataka Wakandarasi kuwasilisha *Annual Returns*. Taaarifa hizi ni muhimu kwani zinaisaidia Bodi na Serikali kwa ujumla, kuweka mikakati ya kuwaendeleza Wakandarasi hususan Wakandarasi wa ndani.

Sita, Sheria ya sasa inatoa mwanya kwa Wakandarasi wa kigeni kuweza kuanza kufanya kazi pasipo kusajiliwa na Bodi.

Saba, Sheria ina upungufu wa kushughulikia Wakandarasi wanaotumia vibaya majina ya makampuni yao kwa kushirikiana na wenye kazi, kuihadaa Bodi kwamba wanafanya kazi hizo wakati hawafanyi kazi hizo.

Nane, Sheria ya sasa haipo wazi namna ambavyo Bodi inaweza kuandaa na kuwasilisha taarifa za utunzaji pesa kwenye Mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili; sehemu ya kwanza Muswada inaweka masharti ya awali kama jina la Sheria na uhusiano na Sheria Kuu, ambayo ndiyo inayofanyiwa marekebisho; na sehemu ya pili ni marekebisho yanayopendekezwa katika vifungu 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya pili ya Muswada, kifungu namba mbili kinahusu kuongeza tafsiri mpya, kama zinavyoonekana katika ukurasa wa 3 – 5 wa Muswada, ambapo kifungu cha pili cha Sheria Kuu kinarekebishwa. Kipengele hiki cha matumizi ya tafsiri ama *application of interpretation* kimeboreshwa. Katika kipengele hiki, masuala ya msingi yametafsiriwa ili kurahisisha uelewa na utekelezaji wa Sheria yenyewe. Maneno hayo ni pamoja na:-

Moja, neno Mkandarasi ama *Contractor*, limepewa tafsiri pana zaidi, ambapo mtu yeyote anayetoa huduma zozote za ujenzi kwa niaba ya mtu mwingine, kwa madhumuni ya kupata malipo au mwekezaji anayejishughulisha na kutoa huduma ya ujenzi anatafsiriwa kuwa Mkandarasi.

Mbili, kazi za miradi ya ujenzi ama *construction works* zitakazofanywa na mkandarasi, zitahusisha pia kipindi cha uangalizi wa mradi ama *defect liability period*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la pili katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 4 (a) mpaka (t), ukurasa wa 5 – 8 wa Muswada, ambapo kifungu cha 4 cha Sheria Kuu kinarekebishwa kwa kuboresha utendaji wa Bodi wa kuiongezea majukumu ili kuipa nguvu ya Kisheria na uwezo wa kudhibiti shughuli za kikandarasi kwa lengo la kuongeza ufanisi zaidi. Majukumu yameongezeka kutoka sita ya Sheria ya sasa hadi kufikia ishirini. Baadhi ya majukumu yaliyoongezwa ni pamoja na yafuatayo:-

Moja, Bodi kuwa na uwezo wa kisheria katika kukagua miradi ili kuhakikisha kuwa kazi za ujenzi zinafanywa na wakandarasi waliosajiliwa na kazi hizo zinafanyika

kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni za nchi, kama njia ya kudhibiti upungufu katika utendaji. Suala hili limefanyiwa marekebisho katika kipengele (c) katika ukurasa wa sita wa Muswada.

Mbili, Bodi kuwa na uwezo wa kisheria wa kuyashtaki makampuni, mashirika au watu binafsi, wanaojishughulisha na kazi za ujenzi bila kusajiliwa kwa mujibu wa sheria. Jukumu hili lipo katika kipengele (d) ukurasa wa saba wa rasimu ya Muswada.

Tatu, Bodi kuwa na uwezo wa kusimamisha mradi au shughuli yoyote ya kikandarasi ama *Issuance of Stop Order*, itakayofanyika bila kuzingatia matakwa ya Sheria hususan pale ambapo usalama wa watu na mali unapokuwa hatardini. Marekebisho yanayoafanywa yapo katika kipengele (p) katika ukurasa wa saba wa Muswada.

Nne, Bodi kuwa na uwezo wa kuweka vigezo vya usajili wa Makandarasi katika madaraja mbalimbali ili kuwawezesha kutekeleza miradi ya ujenzi kikamilifu, jukumu hili limefafanuliwa katika kipengele (l) ukurasa wa saba wa Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tatu katika sehemu ya pili ya Muswada huu, lipo katika kifungu namba nane cha Muswada ambapo kifungu cha tano cha Sheria Kuu, kinarekebishwa kwa kuongeza umuhimu wa kinga kwa *Management*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la nne katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba sita ukurasa wa nane ambapo kifungu cha saba cha Sheria Kuu kinarekebishwa. Marekebisho haya yanalenga kuondoa utata wa tafsiri ya kutambua kazi nyingine zinazofanywa na Wakandarasi wengine, zikiwemo kazi za Wakandarasi wa Umeme ama *Electrical Works Contractors*, Makandarasi wa Ufundi wa Mitambo na Wakandarasi Maalum ama *Specialist Contractors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tano katika sehemu ya pili ya Muswada, lipo katika kifungu namba saba ukurasa wa nane, ambapo kifungu cha nane cha Sheria Kuu kinarekebishwa kumtaka Msajili wa Wakandarasi kutangaza kwenye Gazeti la Serikali majina, anuani na mahali, namba ya usajili, daraja la usajili, pamoja na majina na sifa za wabia au wakurugenzi wa mkandarasi mara baada ya kusajiliwa. Lengo ni kuipa Bodi urahisi wa ufuatiliaji wa kampuni husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la sita katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba nane ukurasa wa tisa, ambapo kifungu cha tisa cha Sheria kuu kinarekebishwa kutokana na makosa ya uchapishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la saba katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba tisa ukurasa wa tisa, ambapo kifungu cha 10 cha Sheria Kuu kinarekebishwa ili kuongeza sifa za maombi ya usajili wa Wakandarasi, likiwemo suala la uzoefu wa kazi za ujenzi na pia sifa nyingine kama zitakavyoainishwa na Bodi. Aidha, usajili huo pia utaambatanishwa na Cheti cha Usajili wa Biashara kilichoidhinishwa na Mamlaka husika hasa BRELA.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la nane katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 10 ukurasa wa 10, ambapo kifungu kipya cha 10A cha Sheria kitaongezwa. Kifungu hicho kipya kinakataza mtu au kampuni yoyote, kujihusisha katika kazi za ujenzi isipokuwa mtu huyo au kampuni hiyo iwe imesajiliwa na Bodi kisheria na iwe imepata cheti cha usajili kinachotambuliwa na Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 9 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo kifungu namba 11 ukurasa wa 10, ambapo kifungu cha 11 cha Sheria kuu kinarekebishwa kwa ajili ya kuboresha Mamlaka ya Bodi katika kutoa usajili wa muda, ikiwepo na kuongeza muda ama *renewal*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 10 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 12 ukurasa wa 10, ambapo kifungu cha 12 cha Sheria Kuu kinarekebishwa kwa kumtaka mtu au kampuni au taasisi yoyote, inayompa kazi mtu au kampuni ya nje ambayo haijasajiliwa, kuwa na wajibu wa kuhakikisha kampuni husika inasajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 11 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo kifungu namba 13 ukurasa wa 11, ambapo kifungu kipya cha 12A kinamtaka Mkandarasi kutoa taarifa ya mabadiliko ya uongozi wa Wakurugenzi, Wabia au wamiliki wa kampuni kwa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 12 katika sehemu ya 12 ya Muswada lipo katika kifungu namba 14 ukurasa wa 11 wa Muswada, ambapo kifungu cha 13 cha Sheria kuu kinarekebishwa kwa kutoa ufafanuzi zaidi juu ya sababu zinazopelekea Mkandarasi kufutiwa usajili ama kusimamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 13 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 15 ukurasa wa 12, ambapo kifungu cha 14, kifungu kidogo cha 3 cha Sheria Kuu kinarekebishwa ili kuondoa utata ama *clarity of progress*, kuhusiana na faini ambayo mkandarasi aliyefutiwa usajili au kusimamishwa usajili, anapaswa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 14 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu cha 16 ukurasa wa 12 wa Muswada, ambapo kifungu cha 15 kifungu kidogo cha 1 cha Sheria kuu, kinarekebishwa kwa kuondoa Mamlaka ya usajili wa leseni ya biashara uliokuwa unafanywa na Kamati chini ya Wizara ya Biashara. Mamlaka hayo sasa kisheria yapo chini ya Wakala wa Leseni za Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 15 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 17 ukurasa wa 12, ambapo kifungu cha 16 cha Sheria Kuu kinarekebishwa ili kumpa msajili wa Bodi, nguvu za Kisheria za kutoa wito ama *summons* kwa wakosaji. Aidha, kifungu hicho pia kinampa Mamlaka Mwenyekiti ama Makamu Mwenyekiti wa Bodi, kutoa maamuzi au maagizo ya Bodi.



Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 16 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 18 ukurasa wa 12, ambapo kifungu cha 19C kinafutwa ili kupunguza idadi ya Wajumbe na kuipa ufanisi wa kiutendaji, Mamlaka ya Rufaa ama *Appeal Authority*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 17 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 19 ukurasa wa 13, ambapo kifungu cha 21 cha Sheria Kuu kinarekebishwa kwa kufanyiwa masahihisho ya maneno ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 18 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 20 ukurasa wa 13, ambapo kifungu cha 22 cha Sheria Kuu kinarekebishwa ili kumbana Mkandarasi yeyote yule, ambaye ataruhusu ama kula njama na kuachia jina lake litumiwe na mtu au kampuni yoyote ambayo haijasajiliwa na Bodi kutekeleza mradi wa ujenzi, atakuwa ametenda kosa ndani ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 19 katika sehemu ya 19 ya Muswada lipo kifungu namba 21 ukurasa wa 13 – 14, ambapo kifungu cha 23 cha Sheria Kuu kinamtaka mtu au kampuni inayoomba kusajiliwa kama Mkandarasi, angalau mmoja wa wamiliki wa kampuni hiyo awe mtaalamu wa fani ya ujenzi. Mabadiliko yanayopendekezwa yanaendelea kutoa ufafanuzi na msititizo wa umuhimu wa kuwa na mtaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 20 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 22 ukurasa wa 14 – 15, ambapo kifungu cha 26 cha Sheria Kuu kinarekebishwa ili kuweka utaratibu na mtiririko mzuri wa taarifa za mapato na matumizi ya Bodi. Ukaguzi wa hesabu za Bodi na pia kuipa nguvu za kisheria za kuidhinisha taarifa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 21 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 23 ukurasa wa 15, ambapo kifungu cha 27 cha Sheria Kuu kinafanyiwa masahihisho ya uandishi wa Kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 22 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 24 ukurasa wa 15, ambapo kifungu cha 32 cha Sheria Kuu kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya kidogo D ili kurahisisha ufunguaji wa mashtaka ya jinai kwa ukiukwaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 23 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 25 ukurasa wa 15, ambapo kifungu cha 23 cha Sheria Kuu kinarekebishwa ili kuipa Bodi uwezo wa kumlazimisha kila Mkandarasi kuwasilisha *Annual Returns* kwa nia ya kuainisha upungufu na hatimaye kubuni mikakati ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 24 katika sehemu ya 2 ya Muswada lipo katika kifungu namba 26 ukurasa wa 15, ambapo kifungu cha 34 cha Sheria Kuu

kinarekebishwa ili kuelekeza taratibu na njia za kutoa zuio ama *Stop Orders* kwa Wakandarasi wanaokiuka Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 25 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 27 ukurasa wa 15, ambapo kifungu cha 35 cha Sheria Kuu kinarekebishwa na kinaendelea kutoa msisitizo wa kila mkandarasi kuwasilisha *Annual Returns*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 26 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 28 ukurasa wa 16, ambapo kifungu kipyua cha 35A cha Sheria Kuu kinaendelea kutoa msisitizo juu ya kufunga mradi mara inapodhihirika kwamba, kazi za mradi wa ujenzi zinasimamiwa na kampuni au mtu ambaye hajasajiliwa na Bodi kisheria. Aidha, kifungu hiki kinahusisha faini isiyopungua milioni moja au adhabu ya kifungu cha miaka mitatu kwa mkosaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la 27 katika sehemu ya pili ya Muswada lipo katika kifungu namba 29 ukurasa wa 16, linahusu marekebisho ya jedwali la Sheria ama *Amendment of Schedule* katika kifungu namba 1(1)(b), ambalo linapendekeza kwamba uwakilishi wa Wakandarasi kwenye Bodi uongezeke kutoka Mjumbe mmoja hadi Wajumbe wawili kwa nia ya kuongeza uwakilishi zaidi kwa maslahi ya Wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Bunge lako Tukufu; Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Muswada huu kwenye kikao cha Wadau ama *Public Hearing*; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa rasimu ya Muswada huu, pamoja na jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa, Bunge lako Tukufu litajadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wakandarasi wa Mwaka 2008 ama *The Contractors Registration Amendment Act, 2008* na kuuboresha na hatimaye kuupitisha ili kuwezesha Sheria mpya ikidhi mabadiliko ya kisera, kiuchumi na mabadiliko ya kiteknolojia yanayoendelea kutokea nchini na duniani katika masuala ya kikandarasi. Hii ina maana kuwa, masuala ya usimamizi, uratibu na uendelezaji wa Wakandarasi nchini, yatafanyika chini ya Sheria iliyo bora na hivyo kuleta ufanisi katika sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naombakutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono na sasa nitamwita Msemaji wa Kamati iliyohusika na Muswada huu ama mwakilishi wake, Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, kwanza, naomba nitoe pole kwa Uongozi wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Rukwa, kwa kifo cha Katibu wa Vijana, Ndugu Christine Yongoro, kilichotokea juzi usiku huko Sumbawanga Vijijini. Naomba Mwenyezi Mungu, aiweke Roho ya Marehemu Mahali Pema Peponi, amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wakandarasi wa Mwaka 2008 (*The Contractors Registration Amendment Act, 2008*), kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 70(2), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Kumi na Tatu wa Bunge, Kamati yangu ilifanya kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wakandarasi wa Mwaka 2008. Napenda kuchukua fursa hii kueleza kuwa, Kamati yangu ilitekeleza kazi hiyo kama ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa kushiriki kwao kikamilifu katika kuupitia na kuujadili kwa ufasaha, Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wakandarasi. Kutokana na umakini wao wakati wa kuujadili Muswada huu, pamoja na wadau na hata katika vikao vya ndani vya Kamati, wameuwezesha Muswada huu kuboreshwa kama inavyojidhihirisha katika jedwali la marekebisho, yaani *Schedule of Amendment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mohamed H. Missanga - Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne K. Malecela - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Ephrahim N. Madeje, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Mheshimiwa Balozzi Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Sigifrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Mwaka A. Ramadhani, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi na Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila anayesoma taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kufanya marekebisho katika Sheria ya Usajili wa Wakandarasi ya Mwaka 1999, ambayo kwa kiasi kikubwa,

imeonyesha upungufu na hivyo kutokidhi mahitaji ya sekta ya ujenzi, kufuatana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Marekebisho ambao utawezesha Sheria ya Usajili wa Wakandarasi kukidhi mahitaji ya Sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ambayo itatumika sambamba na Sheria Mama, pia itahusisha vipengele vinavyolenga kulinda ajira ya wakandarasi wa Kitanzania. Sheria hii itaboresha utendaji wa Bodi kwa kuiongezea majukumu ili kuipa nguvu ya kisheria na uwezo wa kusajili, kusimamia na kujadili shughuli za wakandarasi, ambapo baadhi hufanyika bila kukidhi haja na kutokuwa na vigezo na viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 69(2) ya Kanuni za Bunge za 2004, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau husika wa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wakandarasi ya Mwaka 2008 na kupata maoni na mapendekezo yao. Maoni ya wadau hao, yaliwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 15 Oktoba, 2008 katika kikao kilichofanyika Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawapongeza kwa dhati, wadau walioshiriki katika kuuboresha Muswada huu ambao ni kutoka sekta na taasisi mbalimbali za Kiserikali na zisizo za kiserikali kama vile Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (*CRB*), Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*), Baraza la Taifa la Ujenzi, Chuo cha Uhandisi wa Teknolojia, Chama cha Washauri Tanzania, Wakala wa Majengo Tanzania, Shirika la Viwango Tanzania, Tume ya Udhubiti wa Mawasiliano Tanzania, BRELA, TASECA, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Chama cha Wasafirishaji Tanzania (*TABOA*), Baraza la Mazingira Tanzania (*NEMC*), Mamlaka ya Usafirishaji wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*), Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) na wengineo wengi ambao sitaweza kuwataja wote, lakini wameshiriki kwa namna moja au nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu chini ya Wizara ya Miundombinu, ilifanikiwa pia kuishirikisha Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika kuujadili na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kufanya marekebisho katika Muswada huu kama yanavyojionyesha katika jedwali la marekebisho, ambayo yalipendekezwa yafanyike wakati wa kujadiliwa na Kamati kwa kushirikiana na wadau wote. Muswada huu utaipa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi, mamlaka ya kudhibiti utendaji mzima wa wakandarasi na kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Bodi hii nchini, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii, yanatoa fursa pia kwa wakandarasi kuweza kusimamia na kudhibiti sekta ya ukandarasi na hivyo kupunguza tatizo la Wakandarasi wasiosajiliwa na wasio na ubora na viwango vinavyotakiwa. Aidha, Kamati inaishauri

Serikali kuongeza idadi ya wafanyakazi katika Bodi hii ili iweze kusimamia vyema kazi za wakandarasi wetu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Bodi hii nchini, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii yanatoa fursa pia kwa Wakandarasi kuweza kusimamia na kudhibiti sekta ya ukandarasi na hivyo kupunguza tatizo la Wakandarasi wasiosajiliwa na wasio na ubora na viwango vinavyotakiwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza idadi ya Wafanyakazi katika Bodi hii ili iweze kusimamia vyema kazi za Wakandarasi wetu nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Wakandarasi nchini, kutathmini kwa umakini viwango na sifa za kitaalamu na kitaaluma na kufanya usajili ili kupata Wahandisi wenye sifa na viwango vinavyostahili. Hii itasaidia pia kulipunguzia taifa hasara na kutoa kazi nyingi kwa Wazalendo, ambao kwa namna yoyote ile, gharama zao zitakuwa chini kulinganisha na gharama za Wataalamu kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Muswada huu; katika vifungu vya 34 na 35 vinatoa fursa kwa Waziri mwenye dhamana, kutunga Kanuni na Sheria ndogondogo zitakazoweka utaratibu wa namna ya kuwasimamisha Makandarasi wasiokidhi viwango; Kamati inashauri kuwa ili kulinda taaluma hii na kuepusha maafa kwa watu na mali zao, hatua kali za kinidhamu zichukuliwe kwa wanaokiuka sheria na taratibu zinazowekwa. Bodi inashauriwa pia isisite kufuta usajili kwa Mkandarasi au Kampuni ya Wakandarasi itakayokiuka taratibu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado kuna tatizo la kutokuwa na Wataalamu wa kutosha katika fani ya ukandarasi, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuhamasisha wanafunzi katika Shule za Sekondari, kusoma zaidi masomo ya Hisabati na Sayansi ambayo yatawawezesha kuwa na sifa za kusomea Uhandisi na hivyo kupata Wakandarasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya wataalamu hao nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Makampuni ya Wakandarasi na kwa kupitia vyama vyao mbalimbali vinavyowaunganisha, kutumia mpango wa madaraja unaowekwa na Sheria hii kama changamoto ya kujiendeleza na kukua. Hii ni kwa ajili ya kukabiliana na ushindani wa kibiashara miongoni mwao na hasa kwa Makampuni yanayotoka nje ya nchi.

Kamati inaishauri Serikali kuwawezesha Wakandarasi Wazalendo kupewa kazi kwa upendeleo maalum, hasa kwa miradi inayogharimiwa na Serikali, ili waweze kupata vifaa, mtaji na ushindani wa kibiashara katika Sekta ya Ukandarasi na Ujenzi. Mpango huu utatoa fursa na kuwajengea uwezo Wataalamu Wazalendo katika ushindani, ambao kwa hivi sasa haupo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali iondoe kodi ya vifaa na mitambo ya ujenzi kama ilivyo katika vifaa vya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na marekebisho ya sheria hii, ambayo inatoa fursa kwa Wakandarasi wa kigeni kusajiliwa na Bodi ya Wakandarasi; Kamati inashauri

na kusisitiza kuwa kila kazi itakayotolewa kwa Wakandarasi wa kigeni, Wakandarasi wazalendo washirikishwe katika kazi hizo na watumike sambamba na Wataalamu hao wa kigeni ili kuwajengea uzoefu wa kazi za Kihandisi na Utawala wa Miradi. Aidha, kabla ya Wageni hao kupata usajili, uwepo utaratibu wa kubaini uwezo wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa kabla Idara ya Uhamiaji kutoa vibali kwa wataalamu wa kigeni, yafanyike mawasiliano kati ya Wizara husika na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ili kuona kama wataalamu hao wanafaa na kukidhi viwango vya kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Miundombinu kuongeza juhudi katika kuzisimamia Bodi zake zinazohusika na sekta ya ujenzi, ambazo ni Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*), Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (*CRB*), Bodi ya Usajili ya Wasanifu na Wakadiria Majenzi (*AQSRB*), Baraza la Ujenzi la Taifa (*NCC*), pamoja na Wataalamu wengine, kujenga uhusiano mzuri wa kikazi baina yao ili kazi za sekta ya ujenzi ziwe za viwango na ubora unaokusudiwa. Kamati inaishauri Bodi ya Usajili ya Wakandarasi, kutafuta njia mbadala ya kuongeza mapato yake ili wawe na uwezo wa kufanya maamuzi na kuipunguzia Serikali mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, napenda nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Miundombinu na pia nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Shukuru Jumanne Kawambwa - Waziri wa Miundombinu; Mheshimiwa Hezekiah Nehemia Chibulunje - Naibu Waziri wa Miundombinu; Mhandisi Omar A. Chambo - Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu; Bibi Joyce Mapunjo - Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu, pamoja na Wataalamu na Watendaji wote wa Wizara hii, walioshirikiana na Kamati katika kuandaa na kutoa maelezo ya kina pale yalipohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Johnson P. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Wataalamu wake, kwa kutoa ufafanuzi wa vipengele mbalimbali vya kisheria kwa Kamati yetu. Kamati inawashukuru wadau wote niliokwisha kuwataja hapo awali, kwa ushiriki wao katika *Public Hearing* na kutoa maoni yao, ambayo kwa kweli yamesaidia kurahisisha kazi ya Kamati katika kukamilisha na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Kaimu Katibu wa Bunge - Dr. Thomas D. Kasilillah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii; Bibi Justina Mwaja Shauri na Bwana James John Warburg, kwa kuweza kuihudumia vyema Kamati na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI (K.n.y. MSEMAMI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Miundombinu, Mheshimiwa Kabwe Zitto, napenda kutoa maoni ya Upinzani kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ya Mwaka 2008 (*The Contractors Registration Amendment Act, 2008*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nguvu na ujasiri mkubwa katika kipindi cha miezi miwili iliyopita, ambayo ilikuwa ni ya mapambano makubwa ya kisiasa na hatimaye demokrasia kuchukua ushindi wa kishindo. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007, napenda kutoa maoni kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ya Mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa shukrani na pongezi nyingi kwa Wananchi wa Jimbo la Tarime, kwa kuonyesha dhahiri kuwa haki haiwezi kuthamanishwa na fedha na hivyo kufanya maamuzi yao kulingana na matakwa yao.

Baada ya kutoa utangulizi huo, naomba nitoe baadhi ya vifungu ambavyo Kambi ya Upinzani inaona ni bora vifanyiwe marekebisho ili dhana nzima ya marekebisho ya sheria husika iwe na maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 3(b) cha Muswada kinachokifanyia marekebisho kifungu cha pili cha Sheria Mama, neno “*construction works*” limetolewa tafsiri kama “...*dismantling or demolition of: (a) any building, edifice, structure, wall, ...* Kifungu kipya cha 10A kinasema kuwa hakuna mtu au kampuni itakayofanya kazi yoyote ya ujenzi (*construction works*), hadi awe au iwe imesajiliwa na Bodi na ina cheti halali cha usajili kutoka BRELA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, atoe ufafanuzi kuhusu maana halisi ya “*any building, any wall, any structure*”. Je, hii ina maana kwamba kama mtu ameamua kuvunja ukuta kama tafsiri ya neno *construction works* ilivyosomeka, inabidi mtu huyo awe amepata cheti kutoka BRELA?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kipya cha tano cha Muswada kinachohusiana na mtumishi wa Bodi kutohusishwa kwa tendo ambalo ametenda kwa nia njema wakati akitimiza wajibu wake. Kambi ya Upinzani inaona kifungu hiki mbali ya kuwa na uwezekano mkubwa kuwanyima haki na kuwasababishia hasara walengwa wa sheria hii, vile vile kinahalalisha uzembe kwa watendaji. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo na adhabu ya kifungu au faini kwa watendaji ambao wanaweza kusababisha mhusika kuwa na manung’uniko kutokana na utendaji mbovu wa watumishi wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 11(b) kinachoongeza kifungu kipya cha (5) kinasema, nanukuu: “*Where the project is executed in phases, the Board may extend the duration of the project, on conditions to be prescribed by the Board.*”

Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, mradi wowote kadiri muda wa kumalizika unavyoongezeka, ndivyo gharama zake zinavyokuwa kubwa na hilo linategemea mkataba kati ya mwenye mradi na mkandarasi. Hivyo, itakuwa vizuri kama sheria ingeweka wazi kuwa pindi Bodi itakapoongeza muda wa mradi kwa mradi unaotekelezwa kwa awamu kuwa gharama zitakazoongezeka zibebwe na upande upi kati ya mkandarasi, Bodi au mteja mwenye mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Muswada huu unataka kuipa Bodi ya Wakandarasi nguvu na udhibiti wa Wakandarasi ili kuleta ufanisi katika sekta nzima ya ujenzi. Kambi ya Upinzani inaona dhana hii inaweza kutimizwa pale tu Muswada huu utakapotambua kuwa kada za usanifu majengo (*Architecture*) na wakadiria majengo (*Quantity Surveyors*) ni muhimu sana katika kutimiza lengo kuu la kuleta ufanisi katika sekta nzima ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali pamoja na Bodi, itilie mkazo mkubwa sana juu ya Wakandarasi kufanya ubia; hili litawasaidia sana katika kuleta ufanisi. Pia Bodi isimamie na kuona kwamba pale ambapo Wakandarasi wa kigeni wanapata kazi, basi wawashirikishe Wakandarasi wa Tanzania; hili litawasaidia Wakandarasi wetu sio tu kuinua mitaji, bali pia wataongeza utaalamu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui mazima ya Muswada huu inaonyesha kuwa ni kudhibiti makampuni ya ujenzi na wataalam waliomo katika taslia hiyo. Kambi ya Upinzani inadhani suala kubwa Bodi linatakiwa kutoa miongozo ya uendeshaji (*regulation*), kwa makampuni na wanataaluma wenyewe na si kudhibiti (*control*), ila kama ni kudhibiti haiwezekani Bodi peke yake ikafanya kazi ya kudhibiti bila kuhusisha wasanifu ambao ni *supervisors* wa Wakandarasi. Haiwezekani taslia ya Wakandarasi ikaleta ufanisi unaokusudiwa na Muswada huu bila Wasanifu na Wakadiriaji kutambuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasema hayo kutokana na kifungu cha 4(1)(i) kinachosema nanukuu: “*Furnish managerial, technical and administrative advisory services to contractors.*”

Swali la kuuliza ni kuwa ushauri wa uendeshaji na kiutawala utakaotolewa na Bodi kwa mkandarasi ni kwa malipo au ni majukumu ya Bodi kutoa huduma hiyo? Kama ni kwa malipo ina maana tayari Bodi inakuwa imewafunga wakandarasi wasitafute huduma hiyo pahala pengine ila ni lazima itolewe na Bodi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namheshimu sana rafiki yangu Mheshimiwa Faki. Bahati nzuri tupo kwenye Kamati moja, lakini naomba



Mwongozo wako. Natumia kanuni ya 63 fasili ndogo ya 5, alipokuwa anaanza kuzungumza hotuba yake Mheshimiwa Faki amesema kwamba, anawapongeza Wananchi wa Tarime kwa kufanya uchaguzi mzuri na kwamba haki haiwezi kuthamanishwa na fedha.

Sasa mimi haya maneno ambayo Watanzania wanatusikia, nadhani wanaweza wasijue sawa sawa ni namna gani fedha haiwezi kuthamanishwa na uhuru; nani hasa aliyetumia fedha kule Tarime lakini hakuchaguliwa na huyo ambaye hakutumiwa fedha amechaguliwa?

Naomba mwongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kwa sababu tupo kwenye kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, nitapenda amalize hotuba yake baadaye ajiandae kueleza maana yake ilikuwa nini, lakini amalize hotuba yake kwanza.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa ujumla, Kambi inataka kuishauri Serikali na Bodi, kama kweli inataka na imedhamiria kuwainua Wakandarasi wazalendo, izuie Wakandarasi wa kigeni kushiriki katika *tendering work* za *foreign donors*. Ile Misaada/Mikopo ambayo inalazimisha Wakandarasi watoke nje, sasa huu ni muda muafaka wa Tanzania kama nchi kusema hapana.

Kambi inatoa ushauri huu kwa imani kuwa fedha zinazotolewa na wahisani ni kwa ajili ya Watanzania na hivyo zinatakiwa ziwanufaishe Watanzania wenyewe. Njia hii itazijengea uwezo kandarasi zetu na hata kuweza kushindana nje ya nchi. Aidha, hii itaondoa kasumba iliyojengeka miongoni mwetu kuwa kazi yoyote nzuri haiwezi kufanywa na Mtanzania; hii ni kutokuthamini vipaji tulivyonavyo (hatuthaminiani).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa Taarifa ya Ukaguzi wa Majengo ya Dar es Salaam kama ilivyotayarishwa na Tume iliyoundwa na Waziri Mkuu aliyejiuzulu, Mheshimiwa Edward Lowassa iko wapi; ni sababu gani za msingi zimesababisha Taarifa hiyo isiwekwe wazi kwa ajli ya Watanzania na wadau wengine waliomo katika Sekta ya Ujezi kuiona na kutoa maoni na kufuata ushauri wa Tume hiyo? Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, aitoe kwenye makabati Taarifa hiyo ili fedha za walipa kodi zionekane kuwa kweli zilitumiwa vizuri na kwamba hapakuwa na ufiadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Kambi ya Upinzani inaona huu ni muda muafaka kwa Serikali kuleta Bungeni *Building Control Bill*, ili kuondokana na maafa ya kuporomoka kwa majengo yanayoendelea kuinnyemelea miji mikubwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante lakini pia unatakiwa ueleze sasa ulikuwa na maana gani wakati ule; maneno yako ya kufungua hotuba yalikuwa na maana gani naulizwa?

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa sina zaidi ila kikawaida tu kwamba, uchaguzi una gharama; ni hilo tu basi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kusema kwamba, tunaposema Bungeni tujue kuwa tunautangazia ulimwengu. Kwa hiyo, *statements* zetu ziwe na vithibitisho vinginevyo wananchi hawatuelewi.

Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji inaonekana sio kubwa. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Zambi, atachangia kwanza halafu Mheshimiwa Benito Malangalila atakuwa wa pili.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mchangiaji wa kwanza, lakini pia naomba niseme kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ambapo kwa sehemu kubwa sana nimehusika katika utayarishaji wa Muswada wenyewe. Kwa hiyo, kwa sababu maoni ya Kamati yameshatolewa ambayo mimi ni sehemu yake, mchango wangu utakuwa katika maeneo machache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, niseme kwamba Muswada huu kwanza utaweka au utaipa nguvu sana Bodi hii ya Wakandarasi kwa maana ya kwamba, Muswada wenyewe umekuwa na marekebisho maeneo mengi ambayo yalikuwa hayapo kwenye sheria ile mama. Sasa tunaomba Bodi itumie vizuri fursa hii ya sheria mpya ambayo inakuja. Nina mambo nadhani mawili tu ambayo kimsingi nahitaji ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri.

Jambo la kwanza tuna vyombo vingi ambavyo vinahusika sana na sekta ya ujenzi nchini. Kwa mfano, tuna Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*), Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (*CRB*), Bodi ya Usajili ya Usanifu na Ukadiriaji Majenzi (*AQSRB*) na Baraza la Ujenzi la Taifa (*MCC*). Nadhani hizo ndizo taasisi ambazo zinajihusisha moja kwa moja na sekta ya ujenzi. Nimekuwa napata tabu kwamba ni nani hasa au ni chombo gani hasa ambacho ndio *overall* katika vyombo hivi vyote; chombo kipi kinawajibika kwa mwenzake? Wasi wasi wangu ni kwamba, kila chombo kikifanya kazi peke yake, hapa ndipo tunapopata utata kwa kuwa kazi hizi nyingi zinashabihiana, kusipokuwa na chombo kimojawapo ambacho kitahusika tunaweza kupata tabu sana katika utekelezaji.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri anifafanulie; je ni Wizara yake na kama ni Wizara yake, inahusika vipi katika kuunganisha wajenzi wote? Maoni yangu namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atueleze na kama hakuna hicho chombo basi Wizara ione kwamba, kuna umuhimu wa kuunda chombo hicho. Najua kuna Baraza la Ujenzi la Taifa *National Construction Council (NCC)*, lakini sijui kama linahusika na kama linahusika, je, linahusika kwa kiasi gani kwa sababu sijaona kama limehusika moja kwa moja katika kuziunganisha hizi taasisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni la Makandarasi wetu. Tumekuwa tunazungumza sana kuwa Wakandarasi wetu uwezo wao ni mdogo. Hapa nina mambo mawili; kwanza, Mheshimiwa Waziri atueleze, tumekuwa tunasema wawezeshwe; Wizara inachukua mikakati gani katika kufanya Wakandarasi hawa wazalendo wanawezeshwa kwa maana ya kuwawezesha wao kama taasisi, waweze kupata mikopo na waweze kununua vifaa ambavyo vinaweza vikawafanya kwanza wawe washindani wa hakika kabisa katika sekta ya ujenzi wanapokuwa wanashindanishwa na sekta nyingine?

Nitoe rai pia kwa Wakandarasi wenyewe, waone haja ya kuunda umoja wao, yaani kitu kama *joint venture* na wakisubiri kusukumwa pengine wanaweza wasifanikiwe sana.

Nafahamu kuwa wana umoja lakini mimi sijaona kama ni mkubwa sana wa kuweza kuwafanya wao waweze kushindana kikamilifu katika sekta ya ujenzi. Matokeo yake tumekuta wao kama ni kandarasi, basi wanapata kandarasi zile za madaraja madogo sana, hawawezi kupata kandarasi za madaraja ya juu kwa sababu tu uwezo wao wa kushindana ni mdogo sana. Kwa hiyo, nilikuwa natoa rai hapo, Wakandarasi hawa waone kwamba wana wajibu wa kuunda umoja ambao utawawezesha sasa kwanza kuweza kupata mikopo na wakipata mikopo waweze kununua vifaa na wakiwa na vifaa waweze pia kushindana kikamilifu katika sekta yote ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze jambo lingine la utendaji kazi kwa ujumla; kama tulivyosema, pengine kuja kwa sheria hii itakuwa ni ukombozi kwa sekta ya ujenzi, bado kazi nyingi zinafanywa chini ya kiwango. Hata kwa zile taasisi ambazo unaweza ukaaona tunafikiria pengine zina vifaa lakini kazi nyingi hazina kile kitu kinachoitwa *value for money*. Kazi nyingi zinazofanywa zipo chini ya kiwango na kwa nini zinakuwa chini ya kiwango? Si suala tu kwamba, watu hawana vifaa; suala ni kwamba mara nyingi uzalendo kwetu haupo. Kazi zinazofanywa kuna vitu vinaitwa *ten percent*, kuna wizi unaotokea; kama ujenzi unahusiana na sementi au nondo basi wizi ni mkubwa sana katika sekta hii. Sasa usimamizi ni wa kiwango cha chini.

Kwa hiyo, naomba Wizara pia iweke mikakati kwenye miradi yote inayohusu ujenzi; uwe ujenzi wa barabara, madaraja, nyumba na uwe ujenzi wa miundombinu yoyote ile, usimamizi uwe wa karibu sana. Tunaweza kufanya yote tukawa na sheria nzuri, Wakandarasi wakawa na vifaa vizuri lakini kama hakuna usimamizi katika suala zima la ujenzi, bado tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Wizara ihusike sana katika usimamizi kwa kazi ambazo zinafanywa na Wakandarasi wetu hapa nchini na hapa ndipo tunapoweza kuwa na kazi ambazo baada ya kufanyika, zitadumu muda mrefu na kwa maana hiyo Serikali haitatumia fedha nyingine katika kipindi kingine cha muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu ya Bunge ambayo imehusika sana katika utayarishaji wa

Muswada huu na kwa maana hiyo, nilitaka nichangie machache niliyoyachangia. Naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaye mchangiaji mwingine mmoja tu aliyebaki, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. Kwa hiyo, kama wengine walifikiria kuna wenzao hawapo mnakaribishwa kuchangia. Huu ni Muswada wa kitaalamu.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kama alivyoeleza mwenzangu aliyetangulia, Mheshimiwa Zamboni na mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ambayo imeandaa Muswada huu kabla haujafikishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo Kamati yetu imesisitiza katika uandaaji wa Muswada huu ni suala la mshikamano kwa Wakandarasi wetu, ambao kwa kiasi kikubwa umeonekana kuna upungufu mkubwa na ndicho chanzo kikubwa cha udhaifu wa Wakandarasi wetu wengi ambao uwezo wake unazidi kushuka chini. Sasa njia pekee ambayo Kamati yetu imeweza kuona ni pamoja na kuishawishi Serikali, ione umuhimu wa kuwashirikisha Wakandarasi wetu katika kazi mbalimbali zinazotolewa na Serikali.

Tumejitahidi kuiomba Serikali iongeze hata kile kiwango cha chini ili Wakandarasi wa hapa nchini waweze kuruhusiwa kufanya kazi. Kwa mfano, sasa hivi inaonekana kwamba *ceiling* ni shilingi bilioni moja, lakini sasa kuna haja kabisa kwa sababu gharama za ujenzi zimepanda sana. Tumeona kwamba, kuna haja ya kupandisha hii *ceiling* kutoka bilioni moja na kufikia hadi shilingi bilioni 20. Wakipata miradi mikubwa mikubwa, kwa namna hii itawawezesha kupata faida ambazo zitajenga uwezo wao wa kitaalamu, vile vile uwezo wao wa kununua vitendeakazi kwa sababu kazi nyingi za kihandisi zinataka mashine ambazo bei yake ni kubwa sana. Kwa hiyo, tunaisihi sana Serikali, ione umuhimu wa kuongeza kima cha chini cha kiwango ambacho Wakandarasi wa hapa nchini wanaweza kuruhusiwa kufanya kazi.

Vile vile kama tulivyoainisha kwamba, kuna haja ya Serikali nayo kuona umuhimu wa kushirikisha Wakandarasi wa hapa nchini katika shughuli au kazi ambazo zinatolewa kwa Wakandarasi wa nje. Katika hili ni lazima tuwe makini sana, kwa sababu Wakandarasi hao wa nje wanaweza kupata. Endapo kazi yao imekuwa si nzuri wakasema kanuni imetulazimisha kuwatumia Wakandarasi wa ndani ambao uwezo wao ni mdogo, ndio maana kazi hii imeharibika. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba, kazi hii ambayo tutawashirikisha hawa Wakandarasi wa ndani kwanza tujiridhishe kwamba wana uwezo wa kutosha kwa maana ya kitaaluma na uwezo wa kifedha, lakini tusitoe tu ushirika huu kwa Wakandarasi wa nje eti tu kwa kuangalia uzalendo wetu, hapo tutakuwa tunajiangusha sisi wenyewe kama nchi. Tusitoe mwanya wowote kwa Wakandarasi wa nje kuharibu kazi. Aidha, kwa makusudi au kwa bahati mbaya, sheria inatulazimisha tuwashirikishe Wakandarasi wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu sana kwa Serikali yetu ni kujaribu kujenga uwezo sio tu wa kifedha, lakini uwezo wa kitaaluma. Njia pekee ambayo tunaweza tukaongeza uwezo wa kitaaluma kwa wataalamu wetu wa Kihandisi ni pamoja na kuhimiza masomo ya sayansi toka ngazi ya Shule za Msingi. Sasa hivi imeonekana kwamba, vijana wengi hawataki kushiriki katika masomo ya sayansi. Sababu kubwa ni mafanikio wanayoyaona wale waliochukua masomo ya sayansi, ambao wanafanya kazi sasa hivi; imeonekana kabisa kwamba, waliochukua masomo ya sayansi na wakaingia kwenye *engineering*, mafanikio yao ya kimaisha yanakuwa chini.

Sasa ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba, inaboresha maslahi ya hao Wahandisi ili iwe kivutio kwa vijana ambao wanataka kuchukua masomo ya sayansi. Kwa kweli inaumiza, kama Mhandisi inamchukua miaka mitano mpaka saba kuhitimu na wakati huo huo mtu aliyechukua masomo ya *Arts* au ya Biashara inamchukua labda miaka mitatu kuhitimu, lakini mafanikio ya kimaslahi yanaonekana kwa huyu mtu aliyechukua masomo ya biashara ni makubwa kuliko aliyesoma miaka mingi. Hili linakatisha tamaa.

Sio siri, sote tumepitia katika mashule mbalimbali na vyo, tumeona kiasi gani vijana waliosoma sayansi na waliokuwa mahiri sana, wanabadilisha mwelekeo kutoka sayansi wanakwenda kwenye masomo ya *Arts*, wakiamini kabisa wakichukua masomo ya *Arts* ni rahisi kufaulu na vile vile ukishafika kazini, wewe ndio unakuwa sasa mtu wa kumpangia yule aliyesoma masomo ya sayansi. Sasa nadhani kuna haja kabisa, kuangalia upya mwelekeo wetu juu ya masomo ya sayansi ili kuleta kichocheo kwa vijana wetu kuyapenda masomo haya ili tuweze kupata Wahandisi wa kutosha siku za usoni. Kinyume cha hivyo, Serikali yetu itabakia na wataalamu wa sanaa na kuanza ku-*import* wataalamu wa sayansi ambao sio mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, mambo mengi niliyachangia wakati wa maandalizi ya Muswada huu. Kwa hiyo ni vyema niseme kwamba, naishia hapo ili nitoe fursa kwa wachangiaji wengine waweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii.  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana. Sasa ungechangia yale uliyochangia huko, wenzako hatukuwepo huko tungefaidika zaidi.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio Muswada huu umekuja kwa wakati kwa upande mwingine, lakini kwa vile una mambo ya kiufundi hasa na muda uliokuja mwanzo umetukosesha nafasi kidogo ya matayarisho madhubuti. Hata hivyo, ningependa nichangie masuala mawili, matatu ya Muswada huu.

Kama Mheshimiwa Waziri alivyopendekeza au alivyosema kwamba, Muswada huu umetokana na Sheria ya Makandarasi Na. 17 ya Mwaka 1977. Kuanzia kipindi hicho mpaka leo ni muda mrefu mno na kuna mabadiliko mengi ya kiutendaji ya kiteknolojia na mambo mengi mno. Hatujachelewa sana kurekebisha masuala haya, tunaelewa kwamba, umekuja kutokana na vikwazo vingi ambavyo tumeviona kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Kuna mifano tuliyoiona ya Wakandarasi waliokuja; ikawa mkandarasi huyo huyo ndiyo *supplier*, haikueleweka na tukapendekeza katika iliyokuwa Kamati Teule kuhusu masuala yaliyojitokeza ya watu kuja kuanza kazi hata kabla hawajasajiliwa. Kwa hiyo, mimi kwa upande mmoja nashukuru kwamba, Serikali imeliona hilo na leo imeleta Muswada huu.

Kwa upande mwingine pia tumejionea matukio ya majengo yaliyoporomoka, ambayo watu binafsi wamepelekwa Mahakamani na Sheria haikuweza kukidhi haja, ndiyo maana tukaona ipo haja ya kuleta sheria hii. Sheria hii imezungumzia masuala ya Wakandarasi tu, haikukidhi haja ya majengo yaliyobomoka; lakini kuna matatizo mengi yaliyochangia; hayo majengo kubomoka mbali na Wakandarasi, matatizo hayo yanachangiwa na vifaa duni au thamani ya vifaa vinavyohusika katika ujenzi vikiwemo nondo, saruji, mbao na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Bajeti kilichopita, tuliwahi kuzungumzia masuala ambayo yanahusiana na TBS kuhusu viwango. Viwango hivi tukienda kwa upande wa TBS, wao wanasema wana-*control* viwango hivi lakini kumejitokeza udhaifu mkubwa wa bidhaa zinazopatikana hapa ukilinganisha na vifaa vinavyotoka nje. Kwa hiyo, tuna wasiwasi kwamba, Sheria hii mbali na kuweka vikwazo na taratibu kwa Makandarasi, pia ingeweza kutazama hali halisi ya viwango vya bidhaa vinavyozalishwa hapa nchini ukilinganisha na bidhaa za nje.

Tumewahi kueleza kwamba, leo ukienda kwenye Soko la Tanzania ukaitizama nondo ya milimita 12 au 16 na nondo ile ile inayotoka nje, utakuta ni dhahiri shahiri kwamba, nondo yetu hailingani. Wakandarasi wetu ukiacha wakubwa, hawa wadogo wadogo ni wangapi wanao uwezo wa kuweza kupima kwamba hiki kiwango cha milimita 12 kimetimia kwenye nondo hii; ni wangapi wanaweza kulinganisha kiwango cha saruji wakawa na vipimo halisi wakaweza kulinganisha saruji yetu na saruji nyingine? Huwa tunategemea TBS yetu itupatie hiyo thamani.

Unapochukua saruji ya nje na ukiilinganisha na saruji ya ndani, ukachukua mfuko mmoja ule ule wa saruji ambao kwa watu wa kawaida unatoa matofali 25 ukatazama *value* au uzima wa tofali la saruji ya kwetu na saruji nyingine, utakuta kuna vitu tofauti. Kwa hiyo, tunaomba Sheria hii pia izingatie viwango hivyo na ikiwa viwango vya vifaa vya ujenzi havikutimia, wakulaumiwa si Mkandarasi peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumetolewa *definition* ya *Contractor*; ni yule anayejenga jengo la zaidi ya ghorofa moja. Je, haya majengo madogo madogo mengine wataitwa akina nani hawa? Ningeomba Mheshimiwa Waziri, alitolee ufafanuzi. Kwa mfano, katika kifungu cha tatu anaposema: “*Any person who for a reward or, other*

*valuable consideration undertakes to carry out and complete any construction works for another person, of any structure situated below, on above the ground or other work connected therewith, where such person undertakes to do any such works.”* Halafu kuna maelezo kwamba, himself supplies the material ... Hizi *definitions* ni kubwa na maelezo yake ni marefu kiasi kwamba huyu ambaye anajenga kwa ajili ya *reward* naye tunamwita *contractor*? Kwa kuwa mtu fulani anamjengea mwingine, aidha, kwa tunzo au jambo lingine lolote, sasa huyu tum- *classify* vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, inafaa Mheshimiwa Waziri atufafanulie hayo na katika maoni ya Kamati ya Miundombinu, wameshauri vizuri sana na yanafaa Mheshimiwa Waziri ayachukue. Tatizo linakuja; kama Kamati itaweka wapi haya maoni na katika kifungu gani? Nafikiri Mheshimiwa Waziri akija, atatuambia maoni ya Kamati ya Miundombinu kwa ujumla wake, yalivyozungumzwa bila ya kutaja kifungu fulani kirekebishwe na atafanya vipi ili yaweze ku-*fit* katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho ni kwamba, marekebisho haya yaliyofanywa yanawafanya Wakandarasi wapya wanapojiunga kupata tabu sana kuweza kutimiza viwango hivi vilivyotajwa. Kwa hiyo, Muswada huu pia ungefikiria hawa wasomi wetu wapya na wao wanapotaka kuanzisha makampuni ya Ukandarasi; je, masharti yao yakidhi viwango vipi? Ili kuwapa motisha Wakandarasi wa nchini, inafaa na wao tuwalee *stage by stage* mpaka waweze kufikia viwango vya ushindani kama wanalivyo Wakandarasi wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru, maana Mheshimiwa Engineer Mnyaa usingesimama ningeshangaa sana. Sasa namwita Mheshimiwa Engineer Fuya Kimbita, atafuatiwa na Mheshimiwa Engineer Malangalila.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, labda niseme tu kwamba, mimi si Engineer ni *Architect* lakini watu wengi wanatuchanganya, kwa sababu sisi ndiyo tunao-*design* halafu Engineer anapata kazi ya kufanya. Nashukuru kwamba, ndiye *Architect* pekee katika Bunge lako Tukufu hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Niseme tu kwamba, ninashukuru Sheria hii imekuja lakini imechelewa kidogo kwa sababu ingekuwapo kabla, matatizo mengi ya ujenzi tunayoyapata hapa nchini labda yasingetokea. Tushukuru kwamba, imekuja na naomba tuiunge mkono na tuombe wenzetu wakaishughulikie haraka ili iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Bodi iliyopo ikiongozwa na Ndugu Mhege. Wamekuwa wakijitahidi sana tangu Bodi hii ianzishwe wamekuwa wakifanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa, lakini kwa sheria hii mpya sasa tunawapa meno au uwezo zaidi katika utendaji wao. Kwa ujumla, naomba niipongeze sana hii Bodi yetu

ya Usajili wa Makandarasi wa Ujenzi kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini sasa tunawaomba wakafanye zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa hii Sheria ninavyoiona kwa haraka ni katika kupambana na utapeli katika *Industry* nzima ya *Construction*. Kumekuwepo na utapeli mwingi sana, kuanzia kwenye vifaa vya ujenzi au *Contractors* wenyewe; mtu hana sifa za kuwa *contractor* lakini maadam amesajiliwa basi anajiita *contractor*, matokeo yake anafanya hizi kazi ambazo tunazona ziko *below standard*. Kwa hiyo, naomba tuitumie Sheria hii vizuri kuwadhibiti vihiyo au watu ambao hawana uwezo kamili katika shughuli za kiujenzi. Utapeli umekuwa mwingi kwa sababu mtu mwingine amekuwa akisema mimi nimeshafanya kazi labda hapa nastaaifu nikaanzishe tu kampuni ya ujenzi ili niweze kupata fedha za haraka. Ukweli ni kwamba, katika kazi za ujenzi si kwamba kuna pesa za haraka ila ni kazi zenye kutumia vichwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kuishauri Serikali au kuungana na ushauri wa Kamati katika kuondoa kodi katika vifaa vya ujenzi. Dunia ya leo ni ya sayansi na teknolojia, vinahitajika vifaa vingi sana vya kitaalam katika kazi zetu za ujenzi. Kwa hiyo, tungeomba Serikali izingatie, iweze kutoa unafuu wa kodi katika vifaa vya ujenzi. Kwa ujmla hiyo itatusaidia katika kuhakikisha gurudumu letu la maendeleo linasonga mbele na kupata kazi ambazo zina viwango na ubora unaokubalika katika shughuli zetu zote za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ninakigusia katika Sheria hii ingawa haitawagusa sana wenzetu wanaosimamia hizi shughuli za ujenzi ni utapeli unaotokea wakati wa taratibu za *tendering*. *Contractor* mwingine anaweza akawa ame-*bid very low* kwa kuhakikisha kwamba, anapata ile kazi lakini anajua atakuja ku-*compensate* wapi; katika mambo ya *variation* kama kuna nyongeza ya kazi au kuna kitu kilikosewa, pale ndipo anatumia ule mwanya katika kupata ile faida yake. Tungeomba haya marekebisho katika Sheria yetu ya Manunuzi si lazima yule anaye-*tender low* ndiyo apewe kazi. Kwa hiyo ni kitu ambacho tunaomba hata Bodi nayo isaidie kushauri kwa kuangalia zaidi ubora wa yule Mhandisi au sifa yake ya nyuma katika utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningepomba wale ambao watapewa kinga katika hawa watendaji wa hii Bodi, wasiitumie vibaya ile kinga kwa maana ya kuwaonea Ma-*contractor* ili akitoka pale hawajibiki labda alifanya kwa maslahi ya ile Bodi, ninaomba ile nafasi wasiitumie vibaya, waitumie vizuri kwa uzalendo zaidi. Naiomba pia Bodi, pale Wakandarasi au *Contractors* wazalendo wanapoungana, basi wasaidiwe zile *joint venture projects*. Bodi ihusike katika kuwawezesha hawa wazalendo ili waweze kufanya zile kazi taratibu, ziende haraka na hatimaye waweze kupata kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea ni kazi zile kubwa au nono wanapata wenzetu wachache sana kutoka nje. Vikazi vidogo vidogo ambavyo thamani yake ni ndogo, ndiyo walala hoi au Watanzania wenzangu wanazipata. Naomba na nawashauri Wakandarasi wale wadogo wadogo waungane, Sheria hii ni nzuri itawasaidia. Waungane kwa pamoja ili waweze kupata zile kazi ambazo tunasema ni kubwa na pale anapopata



kazi, basi tumwombe aifanye kwa ufanisi na kwa kutumia wataalam. Kingine na cha kusisitiza hata kwa Wabunge wenzangu hapa ni kwamba, katika hizi kazi za ujenzi ni muhimu mkatumia wataalam. Ie ya kusema nenda miguu mitatu au minne kushoto hapa, hizo zama zimeshapitwa nyakati zake, matokeo yake unakuja kupata hasara kubwa zaidi kuliko kama ungeweza kumtumia mtaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, lakini kama Mheshimiwa Mnyaa alivyotangulia kusema, hii shughuli imekuja haraka mno. Niliona nitoe hayo maoni machache na kuwapongeza wenzangu wote wa Kamati ya Miundombinu, ambao wameupitia kwa kina pamoja na kushirikisha wadau wengine wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mimi nilikuwa nafikiri *Ma-contractor* hasa kule kwenye barabara za vijijini wana matatizo, wanapewa hela hapa wakifika kule hawana vifaa. Wakisafirisha vifaa kutoka mji mmoja mpaka mwingine inakuwa sawa sawa na fedha walizopewa. Nadhani haya ni maoni ya kuyafanyia kazi, si sehemu ya Sheria. Sasa namwita Mheshimiwa Malangalila.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie mchango mdogo katika Muswada huu wa Bodi ya Usajili wa Ukandarasi katika taifa letu la Tanzania. Kwanza kabisa, napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo sababu za msingi za kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kwanza, naamini kabisa kwamba, Muswada huu ukitekelezeka, utaongeza sana ufanisi wa sekta ya ujenzi katika taifa letu. Pia Muswada huu unapendekeza kwamba Bodi iwe na uwezo wa kumsimamisha Mkandarasi, pale inapojiridhisha kwamba Mkandarasi huyu ameshindwa kabisa kufanya kazi zake. Naamini Bodi itatusaidia sana kujenga miji yetu iwe ya kisasa. Tazama Jiji la Dar es Salaam pale Kariakoo, kuna maghorofa na naamini kabisa yamejengwa kienyeji. Unakuta jengo lina ghorofa kumi, chini yake kuna kibanda na hicho kibanda kimezungukwa na maghorofa mawili au matatu ya namna hii; unatarajia nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, unatarajia mji unaojengwa kwa utaratibu huo, hatima yake itakuwa vipi? Ni dhahiri kwamba, Sheria hii itarekebisha miji yetu mingi hususan ile ambayo tutaendelea kujenga. Sasa hivi katika Jiji la Dar es Salaam, nimeambiwa kuna vitu vinaitwa *satelite cities* au *towns*, yaani miji midogo ambayo itajengwa pembeni mwa Mji wa Dar es Salaam. Sasa mimi napendekeza kwa dhati kabisa kwamba, maghorofa yanayoendelea kujengwa Kariakoo ni vizuri washauriwe wajenge katika hizo *satelite towns*. Huo ni moja ya ushauri wangu. Naishauri Bodi hii ya Wakandarasi ishirikiane sana na Bodi dada, kwa mfano, ipo Bodi ya Usajili wa Wahandasi Tanzania na pia ipo Bodi ya Wasanifu na Wakadiriaji Majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Bodi hizi zote zinafanya kazi za ujenzi, napendekeza kwamba, huu Muswada unaoletwa hapa ingekuwa yote mitatu ijadiliwe kwa pamoja. Naamini kama pendekezo ninalolitoa hapa litatekelezwa, sekta ya ujenzi itaboreka sana; kwa sababu Wakandarasi wao wanasajiliwa lakini hawa si wataalam wa ujenzi. Wataalam wa ujenzi ni Wahandisi na huo ndio ukweli wenyewe. Kwa maana hiyo, bado nasisitiza kwamba, ingekuwa ni vizuri Serikali ingeleta Miswada ya marekebisho ya Bodi zote tatu ili tunapomaliza tuseme kwamba tumemaliza kitu kizima. Tujiridhishe kwamba tumefanya kazi iliyojitosheleza ambayo itajenga miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kazi ya ujenzi au kazi ya Makandarasi imevamiwa. Tuliunga Sheria ya Maduka ya Dawa, nadhani tulisema kwamba huwezi kuwa na duka la dawa kama si mtaalam; lakini sielewi kwa nini Mkandarasi si lazima uwe Mhandisi? Hili ni jambo ambalo linasikitisha sana kwa sababu nchi yetu tumeshasomesha Wahandisi wengi sana. Ninapenda kuishauri Serikali ijaribu kuliona hilo. Hawa Wakandarasi wengi wao wanatumia vyeti vya Wahandisi waliokufa, baadhi yao na wengi wao pia wanatumia vyeti vya Wahandisi ambao hawako *site* kabisa.

Anakuja kwangu mimi Malangalila anasema Bwana naomba unipe cheti chako nampa, anapeleka kwenye Bodi anasema bwana mimi nina kampuni yangu na mmoja wa Wahandisi anaitwa Benito Malangalila. Wanaisajili Kampuni na Bodi wanaamini kuwa yupo Mhandisi Malangalila lakini mimi nipo hapa Bungeni. Mimi najitolea kama mfano; kwa hiyo barabara zetu za huko vijijini tunaona zimejengwa ovyo ovyo, Kampuni haina hata *technician*, yule anayelitwa fundi mchundo hayupo.

Sasa kwa utaratibu huu, hii *industry* itakuwa vipi kama wataalam hawapo na Bodi haina uwezo wa kwenda kukagua huko kwenye *site*? Naishukuru sana Kamati ya Miundombinu, imeishauri Serikali kwamba iajili wataalam wa kutosha wa kwenda kukagua kwenye *site*, kuona kama kweli wapo wataalam wanaosimamia kazi za ujenzi wa barabara na kazi za majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilifanya kazi Ujenzi, nilikuwa nashughulikia mambo ya Barabara. Nilifanya kazi Idara ya Maji, lakini wakati sisi tunafanya kazi *site* ya kujenga barabara, mimi kama Mhandisi nilikuwa nakaa barabarani. Mimi kama *technician* nilikuwa nashinda barabarani na wale vibarua, lakini siku hizi ukipita barabarani huko hakuna Mhandisi, hakuna *technician*! Hawa Wakandarasi wanasema wana Mhandisi, hakuna cha Mhandisi *even technician* hayupo. Sasa tunajenga taifa la namna gani? Ni dhahiri kwamba, tunajenga taifa ambalo mwisho wa siku tunaonekana kwamba tumetumia mabilioni mengi sana ya pesa, lakini kila tulichokijenga ni kitu ambacho hakina faida na si kitu cha kudumu. Sasa matokeo yaki ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni kwamba, Wakandarasi katika taifa hili wengi wao wanafanya kazi chini ya viwango kabisa. Sasa tufanye nini? Ni vizuri tukajiwekea utaratibu kama nilivyosema hapo awali, kama ni barabara ya kitaifa, *Regional Manager* lazima awe na Wahandisi wanaozikagua barabara. Kama ni majengo, Meneja wa Majengo wa Mkoa lazima ahakikishe kwamba kila hatua za ujenzi anazifuata

na anaikagua, lakini pia Mkandarasi mwenyewe lazima ajiridhishe kwamba kazi anayoifanya ina viwango vinavyotakiwa. Naamini tukifuata utaratibu huu tutakwenda.

Nizungumzie mfano wa majengo ya ghorofa; si kweli kwamba kila mahali panaweza kujengwa ghorofa lolote. Kwa sababu ili ghorofa lijengwe, kwanza, lazima ifanyike *soil analysis*. Utafiti wa udongo pale ndiyo utakaokuonyesha *structure*, kwamba msingi lazima uwe na upana kiasi gani, unene kiasi gani na nondo unayoiweka pale kwenye msingi iwe na *size* gani. Sasa mimi sielewi kama Wakandarasi wetu katika taifa hili wanayajua hayo? Kwa sababu kazi yoyote ya ujenzi wa jingo, mtu wa kwanza kuitwa ni *Architect*, mtu wa pili ni *Quantity Surveyor*, mtu wa tatu ni *Structure Engineer*, yeye ndiye anayejua hili jengo msingi wake utajengwaje, nondo zake zitakaaje mtu wa nne anaitwa *Construction Engineer* huyu ndiye anayejenga.

Mtu wa tano anaitwa *Consultant* (Mtaalam Mshauri), kila kazi lazima iwe na *consultant*. Sasa katika taifa letu, hawa *consultant* hatuwatambui na wala hatuwatumii. Tumewasajili wachache lakini hata hawa wachache hawatumiki ipasavyo. Sasa tunayo matatizo mengi sana kwenye barabara zetu za vijijini. Mimi nina barabara yangu inaitwa Mbalamaziwa kwa Twanga, nimepita juzi. Ametafutwa Mkandarasi pale, amesha-*grade*, nilikuwa na dereva wangu anasema amepitisha kiwembe. *Regional Manager* anasema hiyo barabara imeshatengenezwa, lakini nakuhakikishia kwamba, ikinyesha mvua mara moja tu basi madhara yatatokea katika barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitaka Serikali ihakikishe kwamba, inapotoa pesa kwa ajili ya kujenga barabara, ijenge barabara sio kukwaruza kwaruza tu hapana, Wananchi wajiridhishe kweli barabara imejengwa na mimi kama Mbunge Mhandisi nikipita niridhike. Hizi ni pesa za wananchi na wananchi wetu ni maskini sana, inasikitisha sana *industry* hii ya ujenzi haifanyiki kama inavyotakiwa. Mambo mengine yanatia uchungu sana, ukienda katika pesa zilizotumika katika barabara niliyoitolea mfano utashangaa.

**NAIBU SPIKA:** Hawakusikia jina hilo ulisema kwa kihehe.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika ni barabara ya Mbalamaziwa kwa Twanga, *junction* yake ipo pale Malangali kwa wale ambao hawapajui vizuri. Sizungumzii barabara nyingine ni hiyo tu ambayo nimetolea mfano, kwa sababu sio Hotuba ya Waziri wa Miundombinu ila tunazungumzia Bodi ya Usajili wa Makandarasi. Kwa hiyo, ninashauri Bodi ya Makandarasi ijiridhishe kwamba, Wakandarasi wanaofanya kazi wanazopewa wafanye kazi kwa ufanisi ili hatimaye Bodi yenyewe ipate heshima. Itakuwa na heshima gani kama Bodi inasajili Wakandarasi ambao hawafanyi kazi zao inavyotakiwa, ndiyo maana tunalalamika kwa nini wageni wanapewa kazi. Tuwape wazalendo ndiyo nchi yao na ndiyo kazi yao hii.

Pamoja na kwamba mimi mwenyewe ningependa sana wazalendo waendeleo kupewa kazi, lakini ningetaka Bodi ya Wakandarasi ambapo leo tunapitisha Sheria ya Usajili, kwanza ifanye Mkutano nao iwaambie Wakandarasi wa Tanzania kwamba

fanyeni kazi kwa ufanisi ili mpate heshima na mkipata heshima tutaendelea kuwapa kazi. Kama hamfanyi kazi kwa ufanisi ni dhahili kwamba tutaendelea kuwapa wageni, huo ndiyo ukweli wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru na naunga mkono hoja hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita msemaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Peter Serukamba; sijui na yeye ni *Engineer*?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi si *Engineer*. Kwanza, nianze kwa kuunga Mkono hoja hii iliyo mbele yetu na nimpongeze Waziri kwa kuleta mabadiliko ya Sheria hii ambayo kiukweli yamechelewa sana. Nampongeza kwa sababu katika nchi yetu sasa hivi tunatumia pesa nyingi sana katika ujenzi wa barabara. Ukiangalia Bajeti zilizopita, kwa miaka mitano kwenye *Industry* hii ni pesa nyingi sana ambazo zimeingia kwenye kazi hii. Kwa hiyo ilikuwa ni muhimu sana Sheria hii ije mapema ili baadhi ya mambo ambayo wameweza kuyaaanisha yatusaidie sana sisi kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina tatizo moja kubwa ambalo nadhani sasa labda Bodi hii itatusaidia; tunaongelea suala la *empowerment* kwa upana wake, moja ya maeneo ambayo yanaweza kutusaidia katika *empowerment* ni kutumia hawa watu wa CRB kwa sababu wana uwezo sasa wa kisheria, wakifanya hiyo kazi vizuri tutasaidia na sisi kuchangia katika kutoa *empowerment* katika nchi yetu. Leo ukipewa pesa na DANIDA, katika masharti yake Makampuni yao lazima yaombe hiyo kazi. Ni lazima na unakuta kazi zote za DANIDA nyingi zinafanywa na *Consultant* wa kutoka nchi zile zile za kwao za Scandinavia; maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu wanajua tunatoa fedha hii lakini ni njia mojawapo ya kuyasaidia Makampuni yao. Kwa miaka karibu mitano iliyopita, Tanzania tumetumia pesa zetu za ndani nyingi sana kwenye barabara. Naipongeza Serikali, lakini pesa hizo zimekwenda kwa Wachina; si jambo baya lakini bado tungeweka mazingira na pesa hizo nyingi Watanzania wangezifaidi. Ni kwenda kwenye *joint venture* tu, unaweka masharti ili upate kazi hii lazima uwe na Mkandarasi wa Kitanzania uombe nae. Hii ndiyo njia ya *empowerment*. Hatuwezi kuwasaidia wananchi wetu kwa kuwapa pesa hizi, lazima sheria nazo zitusaidie kwa kuwasaidia watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana watu wa CRB watusaidie kwenye hili. Kazi nyingi sana unakuta ni pesa za ndani lakini hizo zote *basically what we are doing* tunakusanya Tanzania, tuna-*transfer* kwenda kwa nchi nyingine, kinachobaki ni kweli tunapata barabara lakini bado tungeweza kupata barabara na watu wetu wangepata pesa. Ie *effect* ingekuwa kubwa kwenye *economy* yetu kama tungekuwa tumewasaidia Wakandarasi wetu, hili ni la msingi sana. Lazima namna ya kuwasaidia iwe kwenye *joint venture*. Suala la pili ambalo ningewaomba watu wa CRB ni *incentive*, kama *Contractor* tunalo tatizo, kama nchi Wakandarasi wetu wengi hawana vifaa na si kwamba hawapendi kuwa na vifaa bali vifaa hivi ni gharama kubwa sana. Wanahitaji kuwa na pesa nyingi sana ili wapate vifaa, seti moja ni hela nyingi sana. Ndiyo maana tunalalamika kwenye

Halmashauri kwamba kazi zao ni *sub-standard* kwa sababu wanatumia majembe hawatunii vifaa vinavyotakiwa kwa ajili ya kazi hiyo na hawana uwezo huo.

Uwezo wanaupataje, lazima Bodi hii itusaidie na Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba, kama mtu analeta mitambo tuwape *incentives*. Tumetoa *incentives* kwenye vitu vingi sana, tunashindwa nini kutoa *incentives* kwa mitambo kuingia Tanzania? Tunasema anayeleta mitambo halipi kodi tutakuwa tumewasaidia. Watu wengi wataweza kuingiza mitambo. Kama makampuni makubwa tunawasaidia kwenye mafuta; tunashindwa nini kuwasaidia watu wetu wa ndani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye migodi ya madini, Wakandarasi wanaofanya kazi kule, wale wa nje mafuta wanayotumia wanapewa nafuu ya kodi lakini ukiwa Mkandarasi wa ndani mafuta unayotumia hakuna nafuu ya kodi. Maana yake ni nini na tunataka kumsaidia nani? Kwa hiyo, mimi nasema lazima Bodi hii itusaidie na tuweze kufanya kazi vizuri zaidi kuwasaidia Wakandarasi wetu. Bila hivyo, tutakuwa tunapeleka pesa nyingi kwenye Mawilaya, mvua ikija inachukua mwaka kesho tunapeleka tena lakini hatutakwenda mbele. Ili tuweze kwenda mbele ni lazima tuwasaidie Wakandarasi wetu na mimi nasema CRB itusaidie ichague Wakandarasi hata 20 tuanze na hao, tuwape uwezo tuwawezeshe wakifanikiwa na ku-*takeoff* ndipo na wengine wataweza kupanda.

Hatuwezi kuwasaidia wote kwa sababu hali ya uchumi haituruhusu, tuanze na wachache. Hatuwezi kuendelea kama hatuwezi ku-*empower middle class* na ndiyo watakaotutoa hapa, maana hawa ndiyo watakaolipa kodi na kutoa ajira na lazima CRB itusaidie. Ninaomba sana wenzetu wa CRB watusaidie. Ninataka tuongee jambo hili, tuna Bodi zaidi ya tatu; kuna ERB, CRB na NCC. Bodi hizi kazi yake ni ushauri kwa kazi zote za ujenzi na mambo haya yote yanayofanyika Tanzania. Yapo mambo yanayofanyika, ukijiuliza unasema tuna tatizo la kuangalia mbele.

Leo hii tunafanya kazi kubwa sana ya kujenga barabara, mimi naomba nitoe mfano wa barabara moja tu ya Nelson Mandela. Barabara hii imejengwa miaka 20 au 25 iliyopita, walijenga *double road* mbili. Waliokuwa wanafikiri wakati ule kwa kuangalia Dar es Salaam itakavyokuwa kwa miaka 25 mbele, leo tunarudia kuijenga barabara ile sisi ambao tunakuja baada ya miaka 25 ya wenzetu, tunajenga kwa *double line* vilevile; maana yake sisi hatufikirii miaka 25 mbele.

Lazima tuanze kufikiria miaka 15 ijayo, kama unaamua leo kuwa-*compensate* watu wafidie leo umalize. Ukiwaacha baada ya miaka kumi gharama zitaongezeka zaidi ya mara nne. Lakini unajiuliza kama wenzetu waliofikiri wazee wetu hawa miaka 25 wakajenga barabara ile wakati huo hakukuwa hata na magari na upande ule wa pili hakukuwa hata na nyumba. Leo barabara ile unakaa saa mbili barabarani, tunarudia tena kupaka rangi nzuri na *invention* yetu ni kuongeza njia ya wapita kwa miguu. Badala ya kusema tunaweka *three or four lines*, ili kuhakikisha watu wanatoka Bandarini, wanakimbia kupeleka mizigo uchumi uweze kukua.

Ilitakiwa tuanze kufikiria leo *double line* kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, lakini napata mashaka kama tunafikiri namna hiyo. Kwa hiyo, naomba Bodi hizi ziisaidie Serikali kuleta mawazo, tuanze kufikiri kama wenzetu, miaka 25 ijayo. Dar es Salaam leo watu wanakaa barabarani saa mbili, tunapoteza kwenye uchumi. Hutuwezi ku-*allow* leo mtu anatoka kazini anakaa barabarani kwa saa tatu, tuna tatizo. Kwa hiyo, ufumbuzi unatoka kwenye hizi Bodi zetu na mawazo mazuri ya kutusaidia ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengi sana tunaweza kuyasema, lakini suala la Wakandarasi kuwasaidia ni la msingi sana. Sheria hii ni nzuri sana, tutaweza humo ndani kuwasajili wale wa nje, wataweka ada watapata fedha kama Bodi na itaendelea kuwepo. Yapo mambo lazima tuyashughulikie, ambapo changamoto za msingi ni kusaidia Wakandarasi wa ndani na si lazima wote, tuanze na wachache kama 20. Kila Mkoa ukipata mmoja akawa mkubwa, ume-*solve* matatizo makubwa sana ya kujenga barabara kwenye Wilaya na Halmashauri zetu. Bila hivyo tutaendelea kutumia mapesa na mengine yataanza kurudi kwa sababu hayataweza kufanya kazi; ni *double standard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema ninaomba watu wa CRB watusaidie na waweze kuwasaidia watu wetu wa ndani ili tuweze kufanya vizuri zaidi.

Baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu alikuwa ndiyo msemaji wetu wa mwisho kwenye Muswada huu. Kama mnavyojua, Muswada ni wa kitaalam na ninawashukuru waliochangia, kama nilivyosema wengi ni *engineers*. Mheshimiwa Serukamba yeye hata kama si Mhandisi lakini kasema mambo mazito, tunamshukuru sana.

Kwa muda uliobaki, tungependa Mheshimiwa Waziri akashauriane na wenzake ili tutakaporudi saa kumi na moja, aweze kututolea majibu ya kitaalam pia. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni

(*Saa 06.59 Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli za Bunge mchana, wasemaji karibu wote walikuwa wamemalizika. Kwa hiyo, nadhani tuanze kwa kuwaruhusu Mawaziri waanze kujibu. Sasa sijui watajibu Mawaziri wote au Naibu Waziri anaanza? Waziri Mtoa Hoja, unayo saa nzima kama unaweza.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi nyingine tena ili niweze kuhitimisha hoja iliyotolewa Bungeni leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwa Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu na waliochangia kwa maandishi. Wote nawashukuru sana, wametusaikia katika kukamilisha marekebishi ya Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kawaida, naomba niwatambue waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ambao ni wafuatao: Mheshimiwa Ludovick J. Mwanzila kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki - Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambani, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mheshimiwa Benito William Malangalila na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyechangia kwa maandishi ni mmoja tu, naye ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba, hoja zilizotolewa ni za msingi na zitasaidia sana katika kuboresha usimamizi wa sheria husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema awali katika hotuba yangu, napenda kurudia kwa kusisitiza madhumuni ya kuleta marekebishi ya sheria hii, kubainisha upungufu wa sheria ya sasa na manufaa yatakayopatikana baada ya Muswada huu kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usajili wa Makandarasi Namba 17 ya Mwaka 1997 (*The Contractors Registration Act, 1997*), ilianza kutumika tarehe 1 Oktoba, 1997. Madhumuni makuu ya Sheria hii ni kuhakikisha kwamba, katika soko huria kazi za ukandarasi zinafanywa na watu wenye uwezo wa kutoa huduma na kazi bora na salama kwa watumiaji na umma kwa ujumla.

Tangu kuanza kutumika kwa sheria hii ni zaidi ya miaka 10 na haijawahi kufanyiwa marekebishi yoyote, pamoja na mabadiliko yote ya kisekta ambayo yametokea tangu kutungwa kwa sheria hii. Bodi ya Usajili wa Makandarasi imepata ufanisi wa kuridhisha katika kusimamia na kuendeleza Makandarasi tangu kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Sheria hii ina upungufu kadhaa ambao kama utaondolewa, ufanisi na usimamizi wa Makandarasi utaimarishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya sasa ina upungufu ufuatao:-

1. Sheria ya sasa haiipi Bodi kama chombo chenye mamlaka katika Uekta ya Ukandarasi, uwezo wa kusajili miradi; hivyo kuzorotesha nguvu za Bodi katika kukagua na kudhibiti matakwa ya sheria katika miradi ya ujenzi.

2. Sheria ya sasa haiipi Bodi Mamlaka ya wazi ya namna ya kusimamisha mafundi wasiosajiliwa ama Makandarasi wasio na uwezo, hususan pale ambapo usalama wa watu na mali zao unapokuwa hatarini. Upungufu huu unaifanya Bodi kukosa nguvu ya usimamizi na uhibititi na hivyo kuhatarisha usalama wa watu na mali zao.

3. Sheria ya sasa inatoa mwanya kwa Makandarasi wa kigeni kuanza kufanya kazi pasipo kusajiliwa na Bodi. Hii inasababisha baadhi ya makampuni ya nje kupewa kazi kabla ya ubora wao kutathminiwa.

4. Sheria haina nguvu kushughulikia makandarasi wanaotumia vibaya majina ya nakampuni yao kwa kushirikiana na wenye kazi kufanya biashara ya ukandarasi kinyume na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya kurekebisha Sheria hii yataleta manufaa makubwa sana katika kusimamia kazi na mwenendo wa makandarasi nchini. Aidha, mabadiliko haya yataipa uwezo Bodi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi hususan katika maeneo yafuatayo:-

1. Kukagua na kuhakiki uwezo wa makandarasi katika utekelezaji wa miradi inayoendelea kama njia ya kudhibiti upungufu katika usimamizi wa miradi ya ujenzi. Sasa Bodi itaweza kukagua miradi wakati inaendelea na kuweza kudhibiti upungufu wowote ambao unajitokeza katika mwendelezo wa ujenzi wa miradi hiyo.

2. Kuwashtaki watuhumiwa wa ukiukwaji wa sheria husika.

3. Kusimamisha mafundi au makampuni ambayo hayajasajiliwa kufanya kazi za ukandarasi kwa lengo la kulinda usalama wa wananchi na usalama wa mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo, sasa napenda kujibu na kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na hoja za Mheshimiwa Mwananzila; kwanza ni kuhusu Serikali kuongeza idadi ya wafanyakazi katika Bodi hii ili iweze kusimamia vyema kazi za makandarasi nchini, tunasema kwamba Serikali itaufanyia kazi ushauri huo. Pili, Bodi ya Makandarasi kufanya tathmini ya viwango na sifa za wataalam na kufanya usajili ili kupata wahandisi wenye viwango vinavyostahili; kwa ufafanuzi ningependa kusema, Serikali kupitia Bodi zake za Usajili wa Wahandisi na Usajili wa Makandarasi, watahakikisha kwamba tathmini inafanywa kuhusu ubora wa viwango vya Wahandisi wanaotumika katika sekta za ujenzi. Hili limeshaanza kufanyiwa kazi hasa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) na hivi karibuni tu wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Mheshimiwa Rais, ametoa changamoto kama hiyo ya kuhakikisha kwamba, Bodi inahakikisha uhai wa Wahandisi hao, isiwe tu kwamba baada ya kupata tu usajili, basi usajili huu ni wa maisha. Hakuna vigezo vyovyote ambavyo vinamfanya msajiliwa ama Mhandisi huyu aliyesajiliwa kupoteza sifa ya kuwa Mhandisi.



Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine; Bodi isisite kufuta usajili wa Makandarasi au makampuni ya ukandarasi yanayofanya kazi chini ya viwango. Hapa ningependa kusema kwamba, Bodi ya Usajili wa Makandarasi imekuwa ikifuta Makandarasi wote ambao wanakiuka sheria na kanuni mbalimbali, ikiwemo ya kufanya kazi chini ya kiwango. Katika mwaka 2007 peke yake, Bodi ilifuta usajili wa jumla ya Makandarasi 304 katika zoezi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ya Mheshimiwa Mwananzila ilihusu kuwahamasisha wanafunzi wa shule za sekondari kusoma masomo ya sayansi na hisabati ili hatimaye tuweze kuongeza idadi ya wahandisi. Hapa ningependa kusema kwamba, Wizara yangu kupitia Bodi ya Wahandisi na Bodi ya Makandarasi, imekuwa ikihamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi ikiwemo kuanzisha kitengo cha ushauri wa wanafunzi wanaosoma masomo ya uhandisi, pamoja na kutoa tuzo mbalimbali kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo ya uhandisi. Hii kazi tutaendelea kuifanya katika Wizara na Bodi zinazosimamiwa na Wizara. Naomba nieleze pia kwamba, Wizara nyingine muhimu kama Wizara ya Elimu ipo pia katika mchakato wa kufanya hivyo. Tayari Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina mkakati maalum wa kupita mashuleni na kuwahamasisha wanafunzi katika shule zao ili waweze kuchukua masomo ya sayansi na *focus* mojawapo ni kupata wanafunzi wa kike kuchukua masomo ya sayansi ili tuwe na idadi kubwa zaidi siyo tu ya wavulana, bali ya wasichana kuchukua masomo ya sayansi na baadae tuwe na wahandisi wa kike na wa kiume katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine; Serikali iondoe kodi ya vifaa na mitambo ya ujenzi kama ilivyo katika vifaa vya kilimo. Hapa ningependa kusema, Wizara yangu kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi, imekamilisha utafiti kuhusu matatizo ya mitambo ya ujenzi nchini. Moja kati ya mapendekezo ya utafiti huo ni kuondoa kodi katika vifaa vya ujenzi wa barabara, pamoja na vipuri vyake. Wizara yangu kwa sasa inayafanyia kazi mapendekezo hayo na tutayatolea maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuwa Serikali ihakikishe kwamba, Makandarasi wa kizalendo wanashirikishwa katika kazi zote zinazofanywa na Makandarasi wa kigeni. Vilevile kabla ya kusajili Makandarasi wa kigeni, tathmini ifanye ili kuweza kubaini uwezo wao wa kazi. Usahauri huu umepokelewa na utazingatiwa. Naomba kusema pia kwamba, Bodi imeshaanza mchakato wa kuyashughulikia masuala haya ikiwemo kuwashirikisha Makandarasi Wazalendo katika kazi kubwa kubwa za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla Idara ya Uhamiaji haijatoa vibali kwa wataalam wa kigeni, tathmini ifanye kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ili kubaini kama wataalam hawa wanakidhi viwango; naomba kusema kwamba, usahauri huu umepokelewa na tutauzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine; Wizara ya Miundombinu iongeze juhudi katika kusimamia Bodi yake katika sekta ya ujenzi. Aidha, ushirikiano kati ya

taasisi hizi uboreshwe ili kazi za ujenzi ziwe na viwango vinavyotakiwa. Ningependa kutoa ufafanuzi kuwa, Taasisi zinazoratibu shughuli za ujenzi nchini zinafanya kazi kwa ushirikiano na Wizara yangu. Wizara yangu itahakikisha kwamba, ushirikiano huu unaboreshwa ili kuleta ufanisi katika sekta za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Weston Zamboni ametoa hoja zifuatazo; Bodi itumie vizuri mabadiliko haya ya sheria ili kuboresha huduma. Ushauri huo umezingatiwa. Pili, ameliza ni chombo gani kinachoratibu shughuli za Taasisi zinazoratibu mwendo wa sekta ya ujenzi, yaani CRB, ERB, AQRB au NCC. Ningependa kutoa ufafanuzi kwamba, vyombo vyote hivi vilivyotajwa vimeanzishwa kwa sheria tofauti na vina majukumu tofauti ambayo kwa ujumla wake, yanasaidia kuratibu shughuli za sekta ya ujenzi. Aidha, vyombo hivi vinaratibiwa kwa pamoja na Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu; Serikali ina mikakati gani kukuza uwezo wa Makandarasi wa Kizalendo; ningependa kutoa ufafanuzi kuwa, Serikali kupitia Bodi ya Makandarasi, imeweka mikakati mbalimbali ya kukuza uwezo wa Makandarasi na baadhi ya mikakati hii ni kama ifuatavyo:-

- Mafunzo endelevu kwa ajili ya Makandarasi (*Sustainable Structure Training Program*). Hili ni jambo ambalo tayari Bodi ya Usajili wa Makandarasi imeanza kulifanyia kazi na imeendelea kulifanyia kazi kwa umakini.
- Kuanzishwa kwa Mfuko unaosaidia kuwapa Makandarasi amana ya fedha (*Contractors Assessment Fund*), ni katika mkakati mwingine ambao tayari umeanza kufanywa kazi na Bodi.
- Utafiti kuhusu matatizo ya mitambo ya ujenzi nchini umekamilika na mapendekezo yanafanywa kazi.
- Mkakati wa makusudi umewekwa wa kuwaendeleza Makandarasi wachache wa Ujenzi wa Barabara ili kuweza kufikia viwango vya Kimataifa. Wizara imeunda *Task Force* kukamilisha Rasimu ya Mradi huu. Bodi tayari ipo katika mchakato na mwezi wa saba mwaka huu ikiwa katika mkutano wake mkubwa, pamoja na Wakandarasi wote, wamepitisha maafikiano ya uchaguzi wa Makandarasi wachache ambao kimakusudi, watafanywa mkakati wa kuweza kuboreshwa na kupandishwa viwango ili waweze kuwa katika viwango vya juu kama vile Makandarasi wa kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Zamboni inahusu kufanyika kwa jitihada za kuhakikisha kwamba, Makandarasi wanaofanya kazi chini ya viwango washughulikiwe. Naomba kusema kwamba, ushauri huu tutauzingatia na tumeupokea. Hoja nyingine; Makandarasi wahamasishwe kufanya kazi kwa ubia. Ningependa kutoa ufafanuzi kwamba, Bodi ya Usajili wa Makandarasi imeweka vigezo kwa ajili ya kusajili makampuni ya Wazalendo yanayotaka kufanya kazi kwa ubia.

Aidha, Bodi imefanya mafunzo kadhaa yanayolenga kuwafundisha Makandarasi jinsi ya kufanya kazi kwa ubia.

Bodi imetambua changamoto iliyokuwepo siyo tu haja ya kufanya kazi kwa ubia, lakini uwoga wa Makandarasi wetu wa Kizalendo kufanya kazi kwa ubia au kutokupenda harakaharaka kufanya kazi kwa ubia. Kwa hiyo, Bodi imelazimika kuingia katika mchakato mrefu ambao umehusisha pia kutoa mafunzo ya namna gani ya kufanya kazi kwa ubia na pia kuondosha wasi wasi kwa Makandarasi wetu katika kufanya kazi kwa ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, ametoa hoja kuwa viwango vya kazi zinazotolewa kwa upendeleo kwa Makandarasi Wazalendo, vipande kutoka bilioni moja mpaka bilioni 20. Naomba kusema kwamba, Wizara itashauriana na *Public Procurement Regulatory Authority* kuangalia jinsi ya kutekeleza ushauri huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mnyaa ametoa hoja kuwa, mabadiliko haya ya sheria hayakugusa suala la ubora wa vifaa vinavyotumika katika ujenzi. Naomba kutoa ufafanuzi kuwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi zenye mamlaka ya kisheria ya kudhibiti ubora wa vifaa kama vile TBS, zitafanya mkakati wa kudhibiti ubora wa vifaa vya ujenzi vinavyotumika hapa nchini kwetu. Pia ametoa hoja kuwa tafsiri ya neno mkandarasi inawachukuliaje wanaofanya kazi za ujenzi wa nyumba ndogo ndogo, pamoja na wale ambao wanajenga pasipokulipwa ujira ama *reward*. Ningependa kutoa ufafanuzi kuwa, sheria hii inahusu wale wanaojenga majengo kwa ajili ya matumizi ya umma kama vile shule, hospitali au majengo ya biashara na kadhalika. Sheria haiwahusu wale wanaojenga nyumba ndogo ndogo kwa ajili ya makazi binafsi na majengo yasiyokuwa ya ghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fuya Kimbita ametoa hoja kwamba, sheria itumike kuwabana wasio na sifa wasijipenyeze kwenye sekta ya ukandarasi. Naomba kusema kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri huo. Pili, ametoa hoja kuwa kinga kwa ajili ya wafanyakazi wa Bodi itumike kwa uangalifu. Napenda pia kusema kwamba, Wizara yangu itazingatia sana ushauri huo. Tatu, ametoa hoja kuwa Bodi iweke kipaumbele katika kuhamasisha Makandarasi kufanya kazi kwa ubia na Makandarasi wa aina hiyo wapewe kipaumbele pale wanapoomba kazi. Kama nilivyosema awali kwamba tayari Bodi ya Makandarasi ina mkakati wa kulifanikisha hili na Wizara yangu itaendelea kuuzingatia ushauri huo na kuendelea kuisimamia Bodi ili iweze kufanikisha suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Benito Malangalila ametoa hoja kuwa Bodi zinazoratibu sekta ya ujenzi; CRB, ERB, AQRB na NCC ziongeze ushirikiano katika kuinua ufanisi katika sekta ya ujenzi. Ningependa kusema kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri huo na kuendelea kuzisimamia Bodi hizo ziweze kufanya kazi kwa ushirikiano na kwa ufanisi. Pia, ametoa hoja kuwa kuna haja ya sheria za taasisi zinazoshughulikia sekta moja zinapofanyiwa mabadiliko, Miswada hiyo iwasilishwe kwa

pamoja. Ningependa kutoa ufafanuzi kuwa, Serikali inaupokea ushauri huo na kuuzingatia. Hata hivyo, tungependa kuliarifua Bunge lako Tukufu kwamba, sheria za *National Construction Council* na *ERB*, tayari zimekwisha wasilishwa kwa jili ya kufanyiwa mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Peter Serukamba, ametoa hoja kuwa kuna haja ya kuwepo mikakati ya makusudi, kuwawezesha Makandarasi Wazalendo waweze kukua na kuweza kushindana na Makandarasi wa kigeni kama vile kuwalazimisha wageni kuingia ubia na wazalendo, pamoja na kufanya kazi kwa ubia.

Ningependa kutoa ufafanuzi kuwa katika kulifanikisha hili, kama nilivyosema awali, tayari Bodi ipo katika mkakati wa kuwawezesha Makandarasi wetu wa kizalendo kukuza uwezo, lakini pia kuangalia uwezekano wa kuwashirikisha Wakandarasi wazalendo katika kazi za Wakandarasi wa kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja ambazo zimetolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Bakari Shamsi Faki na naomba nizataje kama ifuatavyo:-

Ufafanuzi zaidi kuhusu marekebisho yaliyopo katika kifungu cha tatu, ambayo yanajumuisha ubomoaji wa majengo, ukuta na kadhalika. Naomba hapa nitoe ufafanuzi kuwa, sheria hii inalenga majengo yanayotumiwa na umma au yale yanayotakiwa kujengwa na kutumia utaalum wa kihandisi ama *structural design*. Ufafanuzi hauhusishi nyumba za kawaida au za kuishi watu binafsi.

Kuhusu kinga ya watendaji wa Bodi kwamba inaweza kutumika vibaya na hivyo kusababisha manung'uniko kwa wahusika. Ningependa kutoa ufafanuzi kuwa, kifungu hiki kipo kwa ajili ya kuwezesha utendaji na kuondoa hofu kwa watendaji. Hata hivyo, hakiwezi kumfanya mtu asichukuliwe hatua pale atakapotekeleza majukumu yake kwa nia mbaya, bila ya kuzingatia maadili ya kazi na bila kuzingatia utaalum wake. Kwa hiyo, inawapa nguvu wataalam wafanye kazi bila kuwa na hofu, lakini haimkingi kama atafanya kazi yake kipotofu kwa maadili mabaya na kwa nia mbaya.

Kuhusu nyongeza ya muda wa kukamilisha kazi za Mkandarasi ambayo inatolewa na Bodi kwa Mkandarasi aliyesajiliwa kwa muda, hoja ilikuwa nani abebe gharama za kazi hiyo kwa muda ulioongezwa. Napenda kutoa ufafanuzi kuwa kifungu hiki kinalenga kuhakikisha kuwa Mkandarasi anaendelea kuwa Mkandarasi kwa kipindi anachokuwa anatekeleza majukumu ya mwajiri wake na Mkandarasi huyo anaweza kupewa usajili wa nyongeza ya muda kama maombi yamewasilishwa na mwajiri wake ambaye ana mkataba naye.

Katika mazingira haya, suala la malipo litakuwa linafafanuliwa kwenye mkataba wa nyongeza. Aidha, Bodi katika kutoa muda wa nyongeza, imeweka masharti kadhaa kwa kuzingatia taratibu na sheria zake ndogo.

Hoja kuhusu kutambua wataalam kama *architects* ama *quantity surveyors* katika sheria hii ili kuleta ufanisi katika sekta ya ujenzi; naomba kutoa ufafanuzi kwamba, wataalam hawa; *Architects* na *Quantity Surveyors*, wanatambuliwa katika sheria zinazotawala fani zao. Aidha, wataalam hawa wana Bodi inayowasimamia na kuratibu utendaji wao wa kazi kwa mujibu wa Sheria ya *Architects and Quantity Surveyors Registration Act No. 16, 1997*. Hivyo, sheria hii ya Wakandarasi inahusu usajili wa Wakandarasi na mambo mengine yanayohusu ukandarasi. Pamoja na kwamba, taaluma zimegawanyika katika sheria mbalimbali, bado kuna utaratibu mzuri na ushirikiano na ushauriano katika utendaji wa kazi za ujenzi.

Kuhusu Bodi kudhibiti makampuni ya ujenzi na wataalam katika sekta ya ujenzi, badala ya kutoa miongozo ya uendeshaji pamoja na ushauri. Mheshimiwa aliuliza kama majukumu ya kutoa ushauri yanalipiwa na wakandarasi. Naomba nitoe ufafanuzi kwamba, majukumu ya Bodi kama yalivyoainishwa katika kifungu cha nne cha sheria, yanatekelezwa na Bodi kwa kuzingatia taratibu na kanuni zilizopo. Aidha, katika kutekeleza majukumu haya, Bodi inatoa miongozo ya kuwaendeleza wakandarasi.

Kuhusu taarifa ya ukaguzi wa majengo iliyotayarishwa na Tume ya aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, naomba kusema kwamba, suala hili bado lipo mikononi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kurekebisha Muswada wa Sheria (*Building Control Bill*) ili kuepuka maafa ya kuporomoka kwa majengo. Naomba kutoa ufafanuzi kwamba, mchakato wa maandalizi kuhusu sheria hii bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea pia mchango kwa njia ya maandishi na hoja hiyo imetolewa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje. Hoja ya kwanza ni ya Makandarasi kushindwa kutekeleza majukumu kutokana na uwezo mdogo wa kununua mitambo. Alitoa ushauri kwa Serikali kuona uwezekano wa kuwasaidia wakandarasi hao. Naomba kutoa ufafanuzi kwamba, ushauri huu ni mzuri na tutaendelea kulitekeleza hili kama nilivyosema awali, kupitia utafiti ambao umeshafanywa na mapendekezo kuwasilishwa Wizarani na sisi tutajitahidi kutolea maamuzi mapema.

Hoja ya pili kuhusu kuwaondolea kodi wakandarasi wanaohangaika kukodisha mitambo ili mitambo hiyo iingizwe nchini na ipatikane kwa gharama nafuu; naomba kutoa ufafanuzi kwamba, ushauri huu umepokelewa na Wizara na itafanya mawasiliano na Wizara husika ili kuona uwezekano wa utekelezaji wa ushauri huo. Kama nilivyoeleza kwa kirefu katika hoja zinazofanana na hiyo huko nyuma kwamba hii ipo katika mchakato na tutaifanyia kazi kikamilifu kuhakikisha kwamba, tunaondosha kero hii na kuwawezesha Makandarasi kufanya kazi zao za ujenzi kwa umahiri na kwa ukamilifu, kwa kutumia vifaa vyenye ubora wa kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ambayo imetolewa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge ni kama hiyo ambayo nimeitolea ufafanuzi. Naomba nichukue nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

## **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

### **Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Usajili wa Makandarasi wa Mwaka 2008 (*The Contractors Registration (Amendment) Bill, 2008*)**

Ibara ya 1  
Ibara ya 2

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 3  
Ibara ya 4

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 5  
Ibara ya 6  
Ibara ya 7  
Ibara ya 8  
Ibara ya 9  
Ibara ya 10  
Ibara ya 11

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 12  
Ibara ya 13  
Ibara ya 14

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Ibara ya 15

(*Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 16  
Ibara ya 17  
Ibara ya 18

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20  
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 22  
Ibara ya 23  
Ibara ya 24  
Ibara ya 25  
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29  
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Usajili wa Makandarasi wa Mwaka 2008 (*The Contractors Registration (Amendment) Bill, 2008*)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Usajili wa Makandarasi (*Contractors Registration (Amendment) Act, 2008*), pamoja na mabadiliko yake, kifungu kwa kifungu na kuukubali.

Hivyo basi, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada huo sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tumekamilisha hatua zote za Muswada. Shughuli zote tulizokuwa nazo kwenye *Order Paper* ya leo zimekwisha. Kama nilivyosema toka asubuhi, Muswada huu umejaa utaalumu sana na naishukuru sana Kamati imefanya kazi nzuri, hata marekebisho yake ni machache.

Mainjia wote waliochangia, wametupa mwanya na wametupa maarifa makubwa sisi wengine wote. Kwa hiyo, hatuna shughuli nyingine katika *Order Paper* ya leo. Kesho tumeona tuanze na Taarifa ya Madini ya Serikali na vitabu vile mlipewa Waheshimiwa Wabunge, sasa msiseme hamna maana havipo. Kwa hiyo, kesho Serikali itawasilisha, iliwekwa Mezani, kwa vyovyote ilikuwa *public document*. Kwa hiyo, Serikali yenyewe siyo kwamba imewasilisha halafu inyamaze, itasema kidogo yaliyomo mle ndani, Kamati iliyohusika ita-*react* kidogo, halafu tutafika mahali.

Nina hakika Serikali itakuwa imetoa mapendekezo ya namna ya kuendelea na shughuli ile, baada ya wao kuwa wameipitia na Kamati ile imepitia. Kwa hiyo, nawataarifu hivi kwa kuwa kesho tutakuwa na maswali, halafu tutaingia katika Taarifa hiyo, mjiandae.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.40 jioni, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,  
Tarehe 29 Oktoba, 2008 Saa 3.00 Asubuhi)*